**INTERNATIONAL MISSIONARY SOCIETY**
**SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH REFORM MOVEMENT**
**General Conference**

625 West Avenue • Cedartown, GA 30125 • U.S.A.
P.O. Box S • Cedartown, GA 30125 • U.S.A.
Telephone (+1) 770-748-0077 • FAX (+1) 770-748-0095
E-mail info@sda1844.org

---

**INTERNATIONAL MISSIONARY SOCIETY**
**SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH REFORM MOVEMENT**
**TANZANIAN UNION**

P.O. Box 70908
Email: unoftzimssdarm@yahoo.com
Dar es Salaam Tanzania

biblewell.org

**www.asd1844.org**

*Mwongozo wa Utafiti wa Kibiblia*

# Miguuni Pake Yesu



## Ngazi ya 2

Miguuni Pake Yesu

# Kielezo cha Mada ya Mwongozo wa Utafiti wa Kibiblia

**Ngazi ya 1**

- ❑ 1 Tajiri Asiyejitambua
- ❑ 2 Je, Yawezekana Kuufahamu Wakati Ujao?
- ❑ 3 Chanzo cha Maumivu Mengi ni Nini?
- ❑ 4 Hatua Nne Kuelekea kwenye Amani ya Ndani na Furaha
- ❑ 5 Namna ya Kuboresha Utu Wetu
- ❑ 6 Ufumbuzi Bora Zaidi kwenye Matatizo na Yanayonihusu
- ❑ 7 Je, Ni Nani Atakayeitawala Dunia Hatimaye?
- ❑ 8 Sababu za Mashaka ya Dunia Yaliyopo
- ❑ 9 Tukio Kubwa Zaidi la Milenia ya Tatu

**Ngazi ya 2**

- ❑ 10 Siri ya lile Sanduku la Dhahabu la Agano
- ❑ 11 Mfumo wa Maisha Unaoleta Usalama na Amani
- ❑ 12 Kumi Kutoa Moja ni Sifuri
- ❑ 12a Kioo na Kivuli
- ❑ 13 Njia Bora Zaidi ya Kuushinda Msongo
- ❑ 14 Udanganyifu Mbaya Zaidi katika Historia
- ❑ 15 Viwango Viwili vya Upendo
- ❑ 16 Je, Kuna Maisha baada Kifo?
- ❑ 17 Ushauri wa Kimbingu dhidi ya Nguvu Zisizoelezeka
- ❑ 18 Kitabu cha Ufunuo na Hatima ya Sayari Yetu
- ❑ 19 Maono Juu ya Ulimwengu Ulio Bora Zaidi

**Ngazi ya 3**

- ❑ 20 Je, Mpinga Kristo Yupo Tayari?
- ❑ 21 Unabii wa Kushangaza wa Miaka 2,300
- ❑ 22 Utetezi Wangu Mbele ya ile Mahakama Kuu
- ❑ 23 Je, ni Kwa Nini Kumekuwako na Dini Nyingi Sana?
- ❑ 24 666 na Marekani Katika Unabii
- ❑ 25 Siku ya Muhimu Zaidi Katika Maisha ya Mtu
- ❑ 26 Namna ya Kumtambua Nabii wa Kweli
- ❑ 27 Funguo Saba Kwenye Maisha ya Kiafya
- ❑ 28 Namna ya Kutatua Matatizo Yangu ya Kifedha
- ❑ 29 Uzuri Halisi
- ❑ 30 Siri ya Mafanikio



# Anwani za Mawasiliano

## NORTH AND CENTRAL AMERICA

**Belize**: Email: info@labibliatienerazon.org
**Canada**: www.4truth.ca / Email: mail@4truth.ca
**Jamaica**: Tel.: (+1) 876-489 1658
imssdajamaica@gmail.com
**Puerto Rico**: Tel./Fax: (+1) 787-726-6192
Email: info@labibliatienerazon.org
**USA**: Email: info@sda1888.org
Web: www.sda1888.org
**Other Caribbean Islands**:
info@labibliatienerazon.org

## EUROPE

**Germany:** Tel.: (+49) 5406-8989952
geschaeftsstelle@reform-adventisten.net
**Italy:** Tel.: (+390) 861-781 110
missionicristiane@virgilio.it
**Spain:** Tel.: (+34) 96-151 2844
info@asdimores.org/asdimores@gmail.com
**The Netherlands:** Tel.: (+31) 313-416 222
Rehoboth@ZDAreformatie.org
**United Kingdom:** Tel.: (+44) 7766322052
treasury.bf@hotmail.com

## AFRICA

**Botswana:** imstso1844@gmail.com
**Cameroon:** Cel. & WhatsApp: (+237) 6 5315 6974
imscameroon1994@gmail.com
**Gambia:** imsgambia1914@gmail.com
**Kenya:** Cel.: (+254) 727-928-488
imskenyaunion@gmail.com
**Lesotho:** AfricanDivision@sda1844.org
**Liberia:** Tel.: (+231) 6-530 668
imssdarmlib2009@yahoo.com
**Malawi:** Cel.: (+265) 884 514 363
malawiunion@hotmail.com
**Nigeria:** Tel.: (+234) 803-744-7190
imsnigeriafield@gmail.com
**Rwanda:** Cel.: (+250) 788 660 278
rwanda_field@yahoo.com
**Seychelles:** imsseychelles1888@gmail.com
**Sierra Leone:** inter.miss.sl@gmail.com
**Sudan:** imssdarmssudanfield@yahoo.com
**South Africa:** Tel.: (+27) 76-615-9434
imssouthafricaunion@gmail.com
**Tanzania:** Tel.: (+255) 565 533 298
unoftzimssdarm@yahoo.com
**Uganda:** Cel.: (+256) 772 370 673
uimssda1844@yahoo.com
**Zambia:** Tel.: (+260) 211-282-805
zamunion@gmail.com
**Zimbabwe:** Cel.: (+263) 712 775 775
imssdazimfd@yahoo.com

## ASIA

**Bangladesh:** bangladeshadventistrms@gmail.com
**China:** Tel. & Fax: (+86) 24-2471 8125
ims1888@163.com
**India:** Cel.: (+91) 98-6203-0096
crosswell.rimsu@gmail.com
imsindia@rocketmail.com
**Indonesia:** Tel. & Fax: (+62) 21-860 7244
imssdarmjkt@gmail.com
annabelllgm@gmail.com
**Malaysia:** AsianDivision@sda1844.org
**Myanmar:** AsianDivision@sda1844.org
**Pakistán:** AsianDivision@sda1844.org
**Philippines:** Tel.: (+63) 32-269-1004
AsianDivision@sda1844.org
**South Korea:** Tel.: (+82) 2-220 1233
AsianDivision@sda1844.org
**Sri Lanka:** Tel.: (+94) 777-566 591
AsianDivision@sda1844.org

## PACIFIC

**American Samoa:** Tel.: (+684) 252 1870
sefoims_amsamoa@yahoo.com
**Australia:** Tel.: (+61) 2-9896 0150
OceaniaDivision@sda1844.org
**Cook Islands:** OceaniaDivision@sda1844.org
**Fiji:** Tel.: (+679) 3548477 / Cel.: (+679) 9533988
sanailaravia@yahoo.com
**New Zealand:** Tel.:0 (+64) 3-352 5023
OceaniaDivision@sda1844.org
**Papua New Guinea:** Cel.: (+675) 721 70 825
OceaniaDivision@sda1844.org
**Samoa:** Cel.: (+685) 7208011 / Cel.: (+685) 7249047
OceaniaDivision@sda1844.org

10. Je, zile Amri Kumi zilitanguliwa?

____________________________________________________________

11. Je, ni mambo gani matatu Mungu aliyafanya katika siku ya saba?

a. ______________
b. ______________
c. ______________

12. Je, ni siku ipi ambayo Yesu aliishika takatifu? ______________________

13. Je, Yesu Kristo aliibadili siku ya pumziko kutoka siku ya saba na kuwa siku ya kwanza?

____________________________________________________________

14. Je, Bwana anaiitaje Sabato katika Isaya 58?

____________________________________________________________

15. Amri 4 za mwanzo huonyesha upendo wetu kwa: ______________________

16. Amri 6 zinazosalia huonyesha upendo wetu kwa: ______________________

17. Je, kifo kinafananishwa na nini?

____________________________________________________________

18. Je, mwanadamu anao ufahamu wo wote mautini? ______________________

19. Je, wafu wanaweza kuwasiliana nasi?

____________________________________________________________

20. Je, Biblia inasemaje juu ya wale wanaoshiriki Unajimu?

____________________________________________________________

21. Pale kipindi cha rehema kinapokwisha, kutakuwa na kipindi kikubwa cha

____________________________________________________________

22. Je, dunia itakuwaje katika kipindi kile cha miaka elfu moja?

____________________________________________________________

23. Kwa kulingana na Biblia, kuna mbingu ngapi?

____________________________________________________________

24. Je, ni kitu gani ambacho hakitakuwako katika ile maskani ya mbinguni?

____________________________________________________________

***Mada za Ngazi ya 3:*** *Je, Mpinga-Kristo yupo tayari?; Je, ni kwa nini kuna dini nyingi? 666 na Marekani katika Unabii? Namna ya Kumtambua Nabii wa Kweli; Namna ya Kutatua Matatizo yangu ya Kifedha.*

*Utashangazwa na mada nyinginezo kwa kulingana na usahihi wa kibiblia pamoja na majibu yake juu ya maswali ambayo yamekushangaza. Usizikose!*

# 10 SIRI YA SANDUKU LA DHAHABU A AGANO



Kunako nyakati za zamani, tamaduni mbali mbali, kama vile za Wainka, Waaztek, Wamaya na Wamisri, kulikuwako na hazina ya sanaa zilizotambulika sana. Kaburi la Kimisri la Tuntakhameni lilikuwa ni maalumu, ndani yake mlipatikana kikamilifu vile vilivyokuwemo pale makaburi mengine yalipochimbuliwa.

Kitu kilichostaabisha zaidi lilikuwa ni lile hekalu ambalo Musa alilijenga kule jangwani. Kila chombo, hususani vile vilivyopatikana ndani ya lile Sanduku la Agano, vilikuwa na maana ya kina kabisa. Vile vipimo vyake, vifaa vyake, mahali pake, pamoja na yale maadhimisho yaliyofanywa ndani ya lile hekalu, hivi vyote vilikuwa na siri muhimu sana. Je, kitu hiki kina maana yo yote kwetu sisi?

## WATU WA MUNGU WALIOKOLEWAJE KATIKA ZILE NYAKATI ZA KALE?

1. Mwanadamu alipotenda dhambi alitengwa na Mungu, na kama isingekuwa Mungu kuingilia, alihukumiwa mauti ya milele. Tokea wakati ule na kuendelea, mwelekeo wake asilia ulikuwa ni kutenda dhambi. Alikuwa dhaifu na asiye mwadilifu. Pale Mungu alipomweka mwanadamu katika Edeni, alimwonya kwamba kama angetenda dhambi angekufa. **Je, hili lilitokea mara moja? Je, ni nani aliyekufa mahali pake? Mwanzo 3:21.**

   *Wana kondoo wawili walikufa mahali pa mwanadamu. Adamu na Hawa walipewa ______________ kama mavazi. Walikuwa ni wa badala yake, ishara ya Mwokozi ajaye.*

2. **Je, ni lini ambapo Mungu aliandaa njia ya manusura ili kumwokoa mwanadamu? 1 Petro 1:18-20.** ____________________________________________

3. **Kulikuwa na njia gani pekee ya uombezi wa dhambi? Waebrania 9:22.**

   ____________________________________________________________

   *Hii ndio sababu ya kwamba sadaka yake Habili ilikubaliwa na ile ya Kaini haikukubaliwa. Mungu alimwagiza yule mtu aliyetenda dhambi alete mnyama ili afe mahali pake. Angeweka mikono yake juu ya kile kichwa cha yule mnyama na kuziungama dhambi zake, jambo lililoashiria kuhamishwa kwa dhambi zake kwenda kwa mhanga asiye na hatia.*

## MUNGU AJIFUNUA MWENYEWE KWA MWANADAMU

4. **Mungu aliwatoa Isaraeli kutoka Misri Naye akawaongoza hata nchi ya ahadi kwa namna ya kustaajabisha. Akayafunua mapenzi Yake pamoja na sheria Yake kwao. Je, Mungu katika maono alimwaagiza Musa atengeneze nini? Kutoka 25:8, 40.**

   ____________________________________________________________

5. **Je, vipimo vya ukumbi uliolizunguka hekalu vilikuwa ni vipi? Kutoka 27:9-19.**

   *Ulikuwa na vipimo vifuatavyo: urefu: futi 150 (dhiraa 100) juu ya nguzo ishirini; upana: futi 75 (dhiraa 50) juu ya nguzo 10 za shaba; kimo: futi 7.5. Mtu asingeweza kuchungulia.*

6. **Hekalu hili lilikuwaje?**

   *Hekalu hili, kwa kulingana na Kutoka 26, lilikuwa na vipimo, futi 40.5 urefu wake, upana futi 9, na kimo futi 7.5. Lilitengenezwa kwa mbao ya mti wa mshita zilizofunikwa kwa dhahabu. Ule mti na dhahabu viliashiria muunganiko wa asili ya kibinadamu na ya kiungu ya Kristo. Mti ulimwakilisha Kristo kama mwanadamu. Dhahabu ilimwakilisha Kristo kama Mungu.*

*Lilifunikwa kwa tabaka nne tofauti.*

- Sehemu yake ya nje ilikuwa ni ya ngozi ya pomboo ya kahawia na nyeusi na mwonekano wake haukuwa wa kuvutia sana. Iliwakilisha asili ya Kristo ya kibinadamu.
- Chini ya tabaka hili kulikuwako na ngozi nyingine ya kondoo dume mwekundu iliyowakilisha mateso ya Kristo.
- Tabaka la tatu lilikuwa la manyoya meupe ya mbuzi, yakiwakilisha usafi wa Kristo.
- Ndani, chini ya matabaka haya matatu, kulikuwako na kifuniko cha kitani nyeupe iliyodariziwa kwa rangi ya samawi, zambarau na nyekundu; rangi za kifalme zikimwakilisha Kristo kama Mfalme.

**Lile hekalu liligawanywa sehemu mbili: Mahali Patakatifu na Patakatifu Mno.**

## *VIPENGEE SABA KWA AJILI YA WAKATI WETU*

**7. Lango la ule ukumbi lilikuwa na upana wa futi 27 pamoja na pazia la kitani nyeupe nzuri lililodariziwa kwa rangi ya samawi, zambarau na nyekundu zikining'inia kutoka katika nguzo nne (Kutoka 27:16). Inamwakilisha nani? Yohana 10:9.**

a) Njia pekee ili kwenda kwa Baba. Waefeso 2:18; 1 Timotheo 2:5.

b) Je, ni kwa nini lango hili lilikuwa ni pana sana? Inaonesha upendo wa Mungu na matamanio Yake ya kumwokoa mwanadamu. 1 Timotheo 2:3, 4.

c) **Nguzo nne.** Kristo amejifunua Mwenyewe katika injili hizi nne. Wito Wake unahubiriwa katika pembe nne za dunia.

**8. Madhabahu ya kafara ilikuwa ni kielelezo cha Kalvari (Kutoka 27:1-8). Je, Yohana Mbatizaji alimwitaje Mwokozi? Yohana 1:29. ________________________________**

a) Kafara. Mnyama wa kuchinjwa alipasa kuwa mkamilifu asiye na ila. Aliiwakilisha tabia ya Kristo isiyo na dhambi. 1 Petro 1:9; Waebrania 4:15. Pale mwenye dhambi alipoweka mikono yake juu ya kichwa cha yule mnyama, alizihamisha zile dhambi zake kwenda kwa yule mnyama asiye na hatia, ambaye alikufa mahali pake. Kuna njia moja pekee ya kuepuka yale mauti ya milele, nayo ni kujipatia aliye wa badala afe mahali petu, kafara. Kristo Ndiye alikuwa kafara asiye na hatia aliyekufa pale Kalvari.

b) Zile pembe zilikuwa ni ishara ya nguvu. Ziliwakilisha nguvu ya kafara ya Kristo.



# SOMO LA 10-19

## *MASWALI YA KUTAFAKARI*

Kusudi la maswali haya ya kutafakari ni kuufikia uelewa wako juu ya yale yaliyomo katika masomo hayo ambayo umeyamaliza. Iwapo unapenda, unaweza ukayakamilisha mbele ya mkufunzi huyu na kisha uyapeleke maswali haya uliyoyajibu kwa usahihi. Iwapo una shaka lo lote, yapitie upya masomo yale ama umwulize mkufunzi huyu.

**1. Adamu na Hawa walivikwa na nini? Hii inaashiria nini?**

________________________________________________

**2. Mungu alimtaka Musa ajenge nini?**

________________________________________________

**3. Kile kinara cha taa kinamaanisha nini?**

________________________________________________

**4. Je, ni kitu gani kilikuwa cha muhimu zaidi mle hekaluni?**

________________________________________________

**5. Je, ni kanuni zipi alizopewa mwanadamu pale Edeni?**

________________________________________________

**6. Sheria ni nini?**

________________________________________________

**7. Msingi wa sheria ya Mungu ni nini?**

________________________________________________

**8. Je, tunaweza kununua mbingu kwa kushika sheria? Kazi ya sheria ya Mungu ni ipi?**

________________________________________________

**9. Kuna aina ngapi za sheria?**

________________________________________________

## *NAWEZAJE KUPATA NAFASI MBINGUNI?*

**14. Je, ni kitu gani ambacho napasa kukifanya kwa nafasi ya kwanza? Matendo 16:31.**

______________________________________________________________________

*Umpokee Kristo, kwa njia ya imani, kama Mwokozi wa nafsi yangu na Bwana wa maisha yangu.*

**15. Je, nifanye nini ili nipate uzima wa milele? Yesu alifundisha nini? Mathayo 19:17 (sehemu ya mwisho).**

______________________________________________________________________

*a) Yeye ____________________ atayarithi haya yote (Ufunuo 21:7).*

*b) Hakutakuwako na nafasi kwa waasi kule; ni wale pekee ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima ndio wataweza kufika mahali pale (Ufunuo 21:8, 27).*

*Ambapo neno hili ''tenda'' linapotumika, na iwe wazi kwamba hili silo chimbuko, bali ni matokeo ya wokovu. Ni sifa za Kristo pekee ndio msingi wa wokovu wetu. Kujitoa na kutii kwetu ni wajibu wetu juu ya upendo wa Mungu, Yeye ambaye tumemkubali sio tu kama Mwokozi bali pia kama Bwana wa maisha yetu.*

## *HITIMISHO:*

- Kristo alifanya sehemu Yake pale Kalvari. Yaliyosalia yanategemea juu yako. "Kama mkikubali, mtakula mema ya nchi" (Isaya 1:19).
- Huu sasa ndio wakati wa kufanya maamuzi na kushikamana na mwamba wa wokovu ambao ni Kristo Yesu.
- Kuupokea mwaliko wa Mungu hivi leo! (Waefeso 5:14-17).

*__Uamuzi wangu:__ Ninatamani kushiriki katika nchi iliyo bora.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

**9. Lile birika la shaba: Kutoka 30:17-21 kunatajwa kutakaswa kwa njia ya maji. Je, tufanyeje ili kuzisafisha dhambi zetu? Matendo 22:16.** ______________________________

*Je, ni nani aliye maji ya uzima? Yohana 4:14.* ______________________________

**10. Kile kinara cha taa chenye matawi saba kilipondwa kutoka katika kipande cha dhahabu (Kutoka 25:31-39). Je, nuru hii inamwakilisha nani? Yohana 8:12.**

______________________________________________________________________

a) Mungu hutuangazia sisi nuru kwa njia ya neno Lake. Zaburi 119:105.

b) Yale mafuta huwakilisha Roho Mtakatifu. Zekaria 4:1-6.

c) Kristo anapoishi ndani yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu, sisi tutakuwa ni nuru ya ulimwengu. Mathayo 5:14 -16.

d) Matawi saba yanaliwakilisha kanisa ambalo kwa njia yake Kristo anauangazia ulimwengu nuru. Ufunuo 1:20.

**11. Je, ile meza ya mikate ya wonyesho inamwakilisha nani (Kuotoka 25:24-30)? Yohana 6:15.**

______________________________________________________________________

a) Je, Yesu anatutaka tufanye nini ili kwamba ale pamoja nasi? Ufunuo 3:20. Tunapasa kufungua ______________________________ wa moyo wetu.

b) Anataka kutuboresha sisi kwa njia ya neno Lake na kutusaidia kukua kiroho. Mathayo 4:4.

**12. Ile madhabahu ya kufukiza (Kutoka 30:1-10) inawakilisha nini? Zaburi 141:2; Ufunuo 8:3.**

______________________________________________________________________

a) Ni kwa njia ya Yesu pekee ndipo maombi yetu yaweza kumfikia Baba na kuwa kama manukato ya kuvutia. 1 Yohana 2:1.

b) Uvumba ulifukizwa kila asubuhi na jioni, ukiwakilisha ibada ya asubuhi na jioni.



**13. Kulikuwa na nini nyuma ya pazia katika Patakatifu Mno? Waebrania 9:2-5; Kutoka 25:10-22.**

______________________________________________________________________

a) Sanduku la agano liliashiria kiti cha enzi cha Mungu. Ufunuo 11:19.
b) Zile mbao za Amri Kumi, zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu, zilikuwamo ndani ya lile Sanduku (Kumbukumbu 10:1-5). Ndizo msingi wa kiti cha enzi cha Mungu na mng'ao wa tabia Yake (Zaburi 89:14; 119:172).
c) Kifuniko, kilichofanyizwa kwa dhahabu safi, kiliitwa ni kiti cha rehema.
d) Kilikuwa na makerubi wawili wenye mbawa zilizoinuliwa kuonyesha malaika wanaokizunguka kiti cha enzi cha Mungu.

## *HITIMISHO*

**14. Vyombo katika lile hekalu huonyesha mpango wa Mungu kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Twawezaje kukua karibu zaidi na Yesu? Waebrania 4:16.**

______________________________________________________________________

a) Vitu saba vilivyotajwa hapo juu huonekana katika umbo la msalaba.
b) Vinatukumbusha sisi juu ya:
   1) Lango: Kristo anatuita sisi.
   2) Madhabahu: Kristo alikufa mahali petu.
   3) Bakuli: Kristo anataka kututakasa sisi kutokana na dhambi zote.
   4) Kinara cha taa: Kristo anataka kuyaangazia maisha yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu.
   5) Meza ya mikate ya wonyesho: Kristo anataka kutulea sisi kwa uwepo Wake na kuwasiliana nasi kwa njia ya Neno Lake.
   6) Madhabahu ya kufukiza: Kristo huyawalisilisha maombi yetu kwa Baba.
   7) Sanduku la agano: Linawakilisha kiti cha enzi cha Mungu. Linatuonyesha sisi ya kwamba rehema na sheria Yake ndio misingi ya serikali Yake. Yesu ndio kiini cha Maandiko, aliyeoneshwa katika vivuli vya Agano la Kale, na katika maisha Yake hapa duniani katika Agani Jipya.

*__Uamuzi wangu:__ Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye kiini cha Maandiko na ya kwamba kila kielelezo katika lile hekalu ni mwendelezo ujao wa injili* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

**5. Pale walipotafakari juu ya maskani ya mbinguni kwa jicho la imani, waumini hawa wa kale walisema nini pale walipotafakari maisha yao ya hapa duniani? Waebrania 11:13-16.**

______________________________________________________________________

**6. Ile nchi mpya itakuwaje? Isaya 35:1, 2, 6 (sehemu ya pili), 7.**

- *Hakutakuwako na majangwa mapana ama bahari kubwa sana.*
- *Dunia nzima itakuwa ni bustani yenye uzuri wa kushangaza (Isaya 55:13).*
- *Mauwa mazuri zaidi kuliko mauwa mazuri zaidi tunayoyafahamu (Ufunuo 22:2).*
- *Matunda mazuri ambayo hapana mwanadamu ye yote aliyepata kuyajaribu hapa.*
- *Kijani kibichi kilichokolea sana kuliko kijani ya chemchemi.*
- *Kutakuwako na mito, vijito na maziwa yenye kuangaza kama kioo.*

**7. Je, unabii unasemaje juu ya masikilizano katika jamii ya wanyama? Isaya 11:6-9; 32:17, 18.**

______________________________________________________________________

**8. Je, ni kitu gani ambacho hakitakuwako kule? Isaya 33:24; 35:3-6.**

______________________________________________________________________

**9. Je, kutakuwa na nini badala ya huzuni? Isaya 35:9, 10; 65:17-25.**

______________________________________________________________________

**10. Je, tutafanya kazi ama tutakaa kizembe? Isaya 65:21-23.**

______________________________________________________________________

**11. Yerusalemu Mpya, ule mji mkuu, utakuwaje? Ufunuo 21:1-5, 10-12.**

*a) Kipimo chake "furlong" (1/8 ya maili) 12,000 (mstari 16), ama km 2,200.*
*b) Umejengwa kwa ________________________, sawa na kioo kinachoangaza (mstari 18).*
*c) Ukuta wake una misingi __________________ iliyojengwa kwa mawe ya thamani (mstari 19, 20).*
*d) Milango 12 iliyofanywa kwa lulu kubwa kubwa (mstari 21).*
*e) Hakutakuwako na usiku kwa sababu Kristo atakuwa ndio nuru yao (mstari 23).*
*f) Kutokea katika kile kiti cha enzi cha Mungu kutakuwako na mto wenye maji yenye kuangaza kama kioo yakitiririka na katika kila upande wa mto kuna ule mti wa uzima (Ufunuo 22:1, 2).*
*g) Tutakuwa pamoja na Yesu kwa milele (mstari 3, 4).*

**12. Je, ni katika siku gani ambapo tutakusanyika ili kumwabudu Mungu? Isaya 66:22, 23.**

______________________________________________________________________

**13. Je, twawezaje kufahamu kwamba ahadi hizi zote ni za kweli?**

- Uzitumainie ahadi za Mungu. Hatuzungumzi juu ya mambo ya kubuniwa ama kuwaziwa tu, bali ni juu ya ahadi za Mungu wa upendo.

a) Matabirio 2,300 ambayo yanatimilika mbele ya macho yetu ndio dhamana ya kwamba Mungu wala hasemi uongo.
b) Ile kafara pale Kalvari isingekuwa na maana iwapo neno hili lisingekuwa ni kweli.
c) Pale Kristo ajapo; tutabadilishwa na kuwa viumbe tusiopatwa na umauti (1 Wakorintho 15:51-58).

# 19 MAONO JUU YA ULIMWENGU ULIO BORA ZAIDI



Je, hili ndilo kusudi la Mungu kutuacha sisi katika ulimwengu huu wa mateso?

Kwa wengi, maisha yamegeuka na kuwa jinamizi,

- kwa kadiri wanavyoteseka kwa magonjwa,
- wamejawa na maumivu; kushindania chakula;
- kutoelewana majumbani;
- kukwazwa na wapendwa wao;
- kufanywa watumwa wa kazi.
- Kwa ajili ya sababu nyingine nyingi, maisha yamekuwa ni mzigo mzito.

Je, ni ndoto ngapi ambazo hazikuweza kutimilika!

- Wengi wanapotafuta urafiki na kuishia kwenye kukataliwa.
- Wengine wanatamani kuwa na afya lakini badala yake wanasumbuka na ugonjwa.
- Wengine wanatamani kuwa na makao yao wenyewe, lakini inaonekana kwamba haiwezekani.
- Nasi sote tunatamani kama wapendwa wetu wangekuwa karibu nasi wale ambao kifo kimewaondoa kutoka kwetu.

**1. Mungu ametuahidi makao yasiyo na uvuli. Je, ni lini tutakapoyapokea? Yohana 14:1-3.**

________________________________________________________

- Tutapewa dunia mpya kama ile waliyopewa wazazi wetu wa kwanza (Mwanzo 1:31). Kila kitu kitakuwa ni kizuri ikijumlishwa na mimea, maua, pamoja na wanyama. Tutafurahia amani timilifu pamoja na furaha.
- Mwanadamu alipokea vipawa vinne pale alipoumbwa: uzima wa milele, tabia kamilifu, makao mazuri, utawala juu ya kila kitu.
- Dhambi ikaleta maumivu badala ya vipaji hivi vyote.

**2. Kusudi la kifo cha Kristo lilikuwa ni nini? 1 Yohana 2:25.**

________________________________________________________

- Kwa njia ya Kristo tutaweza kuwa huru kutokana na utumwa wa yule mwovu, na ndani Yake Yeye mambo yote yatakuwa mapya. Isaya 45:22.

## *MBINGU MPYA NA NCHI MPYA ZITAKUWA KAMA NINI?*

**3. Hivi sasa kuna mbingu ngapi, kwa kulingana na Biblia? 2 Wakorintho 12:2-4.**

________________________________________________________

- Mbingu ya kwanza ni anga linayoizunguka dunia-hewa.
- Mbingu ya pili ni anga-anga la nyota (Zaburi 19:1).
- Mbingu ya tatu ni kile kiti cha enzi cha Mungu (1 Wafalme 8:30).

**4. Je, Mungu ametuandalia nini? 1 Wakorintho 2:9.**

________________________________________________________

# 11 MPANGO WA KIMAISHA UNAOKUPA USALAMA NA AMANI



Hapana usalama ama amani katika siku zetu hizi.

- Mauaji pamoja na njaa huitishia dunia.
- Mawakala wa kushurutisha matumizi ya sheria bila ya mafanikio hujaribu kudhibiti mauaji mijini na kuzuwia wizi.
- Wanasaikolojia, pamoja na viongozi wa kidini wanatafuta kupata ufumbuzi wa kuongezeka kwa mashaka ambayo imewakamata mamilioni ya watu, lakini wasipate jibu lo lote. Wanapuuzia chimbuko halisi la machafuko na ufumbuzi wa Mtoaji wa maisha aliouonesha.

**1. Je, ni sababu zipi mbili ambazo zimemleta mwanadamu kwenye ukingo wa machafuko?**

*a) Yeremia 2:13. Wamemwacha* ____________________________ .

*b) Isaya 24:5, 5, 6. Wameziasi* ______________________________.

## *MPANGO WA KIMAISHA KWA AJILI YA FURAHA*

**2. Je, ni kanuni gani alizopewa mwanadamu katika Edeni? Mwanzo 2:17, 18, 3.**

*Kanuni za sheria takatifu ya Mungu zilitolewa pale mwanzoni tu. Mwanadamu aliambiwa, ''usiibe kutoka katika ule mti,'' ''usitamani.'' Ndoa pamoja na siku ya mapumziko vilitolewa, pamoja na vinginevyo. Pasipo na sheria, pasingekuwako na dhambi. Warumi 4:15.*

**3. Je, Mungu aliziandika zile Amri Kumi juu ya nini na aliziandika kwa kitu gani? Kutoka 31:18.**

*Aliziandika juu ya ________________, kitu kigumu zaidi, kilichoashiria umilele. Ni kitu pekee alichokiandika kwa ________________ chake Mwenyewe. Hii inathibitisha _____________ wa sheria Yake.*

**4. Zile mbao mbili za sheria ziliwekwa wapi? Kumbukumbu 10:5.**

*Ndani ya* ________________________________________________

*Zile amri ndio msingi wa serikali ya Mungu na mng'ao wa tabia Yake (Zaburi 89:14).*

| **MUNGU NI:** | **SHERIA YAKE NI:** |
|---|---|
| Upendo (1 Yohana 4:8) | Upendo (Warumi 13:9, 10) |
| Mtakatifu (Isaya 6:3) | Takatifu (Warumi 7:12) |
| Mwenye haki (Zaburi 129:4) | Ya haki (Kumbukumbu 4:8) |
| Mwema (Zaburi 145:9, 17) | Njema (Warumi 7:12) |
| Wa kweli (Zaburi 89:14) | Ya kweli (Malaki 2:6) |
| Mwaminifu (Kumbukumbu 7:9) | Aminifu (Zaburi 111:7) |
| Wa milele (Zaburi 45:6) | Ya milele (Zaburi 111:7, 8) |

**5. Kusudi halisi la ile sheria ni ipi? Warumi 3:20, 31; 7:7.**

*Ile sheria hutufanya sisi kuitambua* ________________________________________

**6. Je, ni kwa njia ya sheria ipi ambayo tutahukumiwa nayo katika ile hukumu ya mwisho? Yakobo 2:10-12**

________________________________________________________

## *MSIMAMO WA YESU KUHUSU ZILE AMRI KUMI ULIKUWAJE?*

**7. Je, ni nani aliyeandika ile sheria pale Mlima Sinai, ni Baba ama ni Mwana? Nehemia 9:12, 13; 1 Wakorintho 10:1-4.** ____________________

**8. Je, unabii ulisemaje juu ya msimamo wa Kristo juu ya sheria?**

*a) Zaburi 40:7, 8. Sheria Yake ____________________ (Yohana 15:10).*

*b) Isaya 42:21. Inasema kuwa Yeye ataitukuza na kuiadhimisha sheria. Tunaposoma Mahubiri ya pale Mlimani, tunaona kuwa unabii huu ukitimilika (Mathayo 5:21, 22, 27, 28, 33-37, 48).*

**9. Je, ni jinsi gani ambavyo alionesha asili ya milele ya ile sheria? Ni nini ambacho kingetokea kwanza? Luka 16:17.**

____________________

**10. Tunathibitishaje katika kumtii Mungu? Yohana 14:15, 21.**

*____________________ wetu Kwake.*

*Agano jipya hutofautiana na lile la kale katika sheria ile ambayo imeandikwa tu juu ya mawe, lakini ni katika mioyo na akili zetu (Waebrania 10:16).*

*Iwapo mtu anasema ya kwamba anaye mke wake moyoni mwake, hapo anamaanisha nini? Je, ina maana ya kwamba anataka kumtaliki?*

**11. Je, Yesu alimjibu nini yule kijana tajiri pale alipouliza kama afanye nini ili kuurithi uzima wa milele? Mathayo 19:16-19.**

*Ukitaka kuingia katika uzima wa milele, ____________________.*

**12. Je, ni nani ambao watashangazwa sana katika ile siku ya hukumu? Mathayo 7:21-23.**

*Wale waliosema kuwa ____________________ nao wasiyafanye ____________________*

**13. Je, yawezekana kuishika sheria ya Mungu?**

*a) Warumi 8:5-8. Wale wayafuatao mambo ya mwili (watu wa kawaida) hawawezi ____________________ .*

*b) 1 Yohana 5:2-3. Upendo wa Mungu unapojaa moyoni mwetu, tunaona ya kwamba amri Zake hizi wala sio ____________________.*

**14. Je, twawezaje kuwatambua wale Wakristo halisi? 1 Yohana 2:3-6.**

____________________

## *HITIMISHO*

Ile sheria ya Mungu ya milele na ikawe ndio mpango wa kimaisha nayo ndio iongoze tabia yetu. Haiwezi kutanguka kama vile alivyo Mungu Mwenyewe.

**15. Je, ni ahadi gani ambayo Mungu awapatia wale wanaozishika amri Zake?**

*a) Kumbukumbu 5:29. Wata____________________.*

*b) Zaburi 119:165. Mioyo yetu itajawa na amani.*

*__Uamuzi wangu:__ Ninakubali ya kwamba zile Amri Kumi ndio tabia ya Mungu na ni msingi wa kiti Chake cha enzi.* ❏ *Ndio* ❏ *Hapana*

b) Udanganyifu mkubwa utafanyika. Ufunuo 20:8, 9.
- Shetani atawahakikishia kwamba yeye ndiye aliyewafufua.
- Atawaambia kwamba wataweza kuuteka ule mji wa Mungu na kuweka ufalme wa kwao wenyewe.

c) Katika wakati ule, kile kiti kikuu cha enzi pamoja na Hakimu wa ulimwengu wote akiketi juu yake, wataonekana. Ufunuo 20:11.
- Kila mwanadamu atayaona maisha yake mwenyewe, kama vile filamu, yakipita mbele ya macho yao.

**16. Je, ni kitu gani kitashuka kutoka mbinguni pale Shetani pamoja na wale waovu watakapojaribu kuushambulia mji ule? Ufunuo 20:9.** ____________________

a) Ile hukumu itakuwa kwa kulingana na kila mtu anavyostahili. Ufunuo 20:13.

b) Mauti ya pili itakuwa ndio ya mwisho. Ufunuo 20:14, 15.

c) Hapatakuwa na shina wala tawi lililoachwa. Kutabakia majivu pekee, jambo ambalo linamaanisha ya kwamba katika kiwango fulani ule moto utazimishwa. Malaki 4:1-3.

**17. Je, Mungu atafanya nini na dunia baada ya kutakaswa kwa njia ya moto? 2 Petro 3:11-13.**

____________________

a) Waliokombolewa wataishi kwa furaha katika dunia mpya kwa milele. Ufunuo 21:3, 4.

b) Mpango wa Mungu wa kurejesha utulivu wa paradiso ya Edeni utatimilika.

## *HITIMISHO*

- Je, wewe utakuwa wapi katika ile miaka elfu - kule mbinguni ama duniani?
- Utakuwa wapi mwishoni mwa milenia-katika Yerusalemu mpya ama miongoni mwa wale watakaoangamia kule nje?
- Katika ule umilele wewe unapanga kuwako wapi?
- Yesu amefanya kila kitu kwa ajili yako. Anataka kukuokoa. Je, utamruhusu afanye hivyo?

*__Uamuzi wangu:__ Ninaamini juu ya maisha ya milele na ya kwamba Mungu atafanya nchi mpya baada ya ile miaka elfu.* ❏ *Ndio* ❏ *Hapana*

**Matukio ya mwisho kwa ufupi:**






# 12 KUMI KUTOA MOJA NI SIFURI 10-1=0

**10-1 unapata nini? Kule shule tulifundishwaje?** Huenda ukasema ni 9, lakini Mungu anasema ya kwamba 10-1=0. Je, sayansi iliyo sahihi imekuwa isiyo sahihi? Hapana, Mungu analo jibu sahihi, ni hesabu katika kipimo kingine.

Wala hili sio jambo lisilo muhimu sana! Furaha yetu binafsi pamoja na ile ya familia, pamoja na ustawi wa mataifa, hutegemea jambo hili. Hata wokovu wetu wenyewe upo mashakani. Mungu hakubaliani na dini ya kubembelezana. Watu wamezowea kubembelezana, na dini za kisasa zinajaribu kufanya masikilizano na Mungu. Wanapenda dini zenye misisimko pasipo kuwajibika, pasipo na utii kwa Mungu, pasipo na kanuni. Wanatarajia kwamba Mungu atafanya mapunguzo na kuamini ya kwamba kama wakishika nyingi katika zile amri basi yatosha kwao kukubaliwa mbele za Mungu. Wanazichukulia zile amri kama vile waonavyo wao wenyewe.

## *HEBU NA TUHESHIMU KILE MUNGU ALICHOSEMA*

**1. Je, Biblia inasemaje juu ya mtu yule anayeikataa yo yote katika zile Amri Kumi? Yakobo 2:10-12.**

______________________________________________

**2. Je, Mungu anasemaje juu ya wale ambao wanadhani ya kwamba wamekuwa ni Wakristo wazuri lakini hawazishiki amri Zake? 1 Yohana 2:3, 4.** ______________________

**3. Je, anasemaje juu ya wale wanaoipanga dini kama vile wapendavyo na kubadili baadhi ya zile amri? Mathayo 15:9.** ______________________________

a) Mungu hajaruhusu badiliko lo lote katika sheria Yake. Kumbukumbu 4:2; Muhubiri 3:14.

b) Hapana hata badiliko dogo liwezalo kufanywa. Mathayo 5:17-19.

c) Hapajawa na sababu ya kubadili kitu cho chote katika ile sheria. Ile sheria ni kamilifu. Zaburi 19:7.

## *LAKINI NI JUU YA SHERIA GANI AMBAYO MAFUNGU HAYA HUELEKEZA?*

*ZILE AMRI KUMI, HAKIKA KAMA ZILIVYOANDIKWA KWA CHANDA CHA MUNGU.*

**4. Ile amri ya kwanza inakataza nini? Kutoka 20:3.**

______________________________________________

*AJua pamoja na sayari nyinginezo zilikuwa zikiabudiwa huko nyuma; na hata sasa watu katika nchi nyingine huabudu wanyama; kwa mfano, ng'ombe hufikiriwa kuwa ni watakatifu kule India. Hivi sasa, tunayo miungu ya kisasa. Kitu cho chote ambacho tunachokiona kuwa ni muhimu kuliko Mungu kinakuwa ni mungu kwetu; kwa mfano, kuishi ili kula badala ya kula ili kuishi (Wafilipi 3:19) ama tunapotoa kipaumbele kwenye starehe, michezo, zawadi, n.k. (Mathayo 10:37), inakuwa ni aina ya ibada ya miungu.*

**5. Je, ile amri ya pili inakataza nini? Kutoka 20:4 -6.**

______________________________________________

*a) Hapa pana sababu ya jambo hili. Kumbukumbu 4:15, 16.*

*b) Yohana 4:24. Mungu anatutaka tumwabudu Yeye katika* ______________________

*c) Je, Biblia inasemaje juu ya ibada ya miungu? Isaya 44:9, 10, 18, 19.*

**6. Je, ile amri ya tatu inakataza nini? Kutoka 20:7.**

______________________________________________

a) Mungu ni mtakatifu Naye anataka kwamba tulichukue jina Lake kwa kicho. Katika Mathayo 5:34-37

tunaona ya kwamba amri hii inakataza pia ________________________________. Isipokuwa tu kiapo cha kisheria (mahakamani).

b) Je, kutatokea nini kwa wale wanaosema maneno ya ovyo? Mathayo 12:36.

**7. Ile amri ya nne inatuamuru tufanye nini? Kutoka 20:8-11.**

________________________________________________________________________

*Ni lazima tufanye kazi katika siku sita za kwanza za juma na kupumzika katika siku ya saba, ndio Sabato. Ni kumbukumbu ya uumbaji, nayo inapasa kuwekwa wakfu kwa ajili ya ibada. Ni kwa ajili ya faida yetu wenyewe. Marko 2:27.*

*Huenda masomaji alipata kujifunza ya kwamba amri ya tatu inasema, "zitakaseni sikukuu." Ama ni kwa sababu gani kuna tofauti juu ya namna ambavyo zile amri zinavyofundishwa? Wale wanaofundisha amri hii kwa namna hii huiruka ile amri ya pili na kuigawanya ile amri ya mwisho iwe ni mbili, ili zipatikane 10. Kuadhimisha "sikukuu" sio sawa na kuiadhimisha siku fulani mahususi. Mungu hajamwidhinisha mwanadamu ye yote kuibadili sheria Yake. Tunapasa kuipokea kama vile ilivyoandikwa katika Biblia.*

**8. Je, ni nani tupasao kuwaheshimu kwa kulingana na amri ya tano? Kutoka 20:12.**

________________________________________________________________________

**9. Amri ya sita inaeleza, "Usiuwe." Kutoka 20:13. Amri hii ina maana gani kwa kulingana na mafundisho ya kiroho ya Kristo?**

*Hatuna haki ya kuondoa uhai wa mtu ye yote, hata wetu sisi wenyewe.*

*a) Mathayo 5:38, 39, 43-45. Wapendeni ________________________________.*

*Yesu Kristo alililifafanua juu ya maana ya kiroho ya amri hii, ambayo inakataza kushiriki katika vita, ambayo ni mauaji makubwa; ni kinyume na mafundisho Yake.*

*b) Mathayo 5:21, 22; 1 Yohana 3:15. Kumchukia mtu, kuapa ama kuweka kinyongo pia ni uvunjaji wa amri hii.*

*c) 1 Wakorintho 3:16, 17. Tusizihalifu zile sheria za ________________________________*

**10. Amri ya saba inasema, "Usizini." Kutoka 20:14.**

*Amri hii inalinda umoja wa familia. Mahusiano yo yote ya kindoa nje ya ndoa Mungu ameyakataa.*

*a) Je, Yesu alisema nini juu ya kutazama na kuwaza kwa kutamani? Mathayo 5:27, 28.*

________________________________________________________________________

*b) Je, ni halali kwetu kuangalia matukio ya ghasia na ukafiri wa kindoa hata kama sio kitu halisi? Wafilipi 4:8.* ________________________________________________________

**11. Amri ya nane inakataza nini? Kutoka 20:15.**

________________________________________________________________________

*Hii inajumuisha namna zote za wizi, ukiwa mkubwa ama mdogo; kama vile kuteka vitani, utumwa, kutokuwa mwaminifu katika biashara, kuchanganya bidhaa, vipimo vya uongo, kutumia nafasi ya kutofahamu ama udhaifu wa mtu mwingine, kuharibu mvuto wa mtu, kutowajibika kazini, mishahara isiyostahili, kwa ujumla ni kila kitu kilicho katika tendo lisilo la uaminifu.*

**12. Amri ya tisa inasema, "Usimshuhudie jirani yako uongo." Kutoka 20:16. Ni nani watakaozuiliwa wokovu? Ufunuo 22:15.**

________________________________________________________________________

*Kila udanganyifu, lau kama kusudi lake ni lipi, umejumuishwa katika amri hii. Twaweza kudanganya kwa kupunga mkono (kuashiria) ama kupepesa, ama kwa kuficha ukweli kwa hiari kwa lengo la kudanganya.*

**6. Baada ya tetemeko kubwa la nchi, ni nini kitawatokea wale waliokufa katika Kristo? Ufunuo 16:18; 1 Wathesalonike 4:16.** ________________________________

- Wale wanaofufuliwa katika ufufuo huu, wanaitwa wenye heri. Ufufuo 20:6.

**7. Kutatokea nini kwa wale waliofufuliwa na wenye haki walio hai pale Yesu ajapo? 1 Wathesalonike 4:17.**

*Watabadilishwa na kuwa katika kutokufa (1 Wakorintho 15:51-54) na ______________________ katika mawingu. Wenye haki watasafiri katika anga hadi kunako makazi ya mbinguni ambako watatawala pamoja na Kristo kwa miaka elfu.*

**8. Kutatokea nini kwa waovu walio hai bado pale Yesu ajapo? 2 Wathesalonike 1:7-9.**

________________________________________________________________________

*Waovu waliokufa watabaki kuwa wafu.*

## *MATUKIO KATIKA ILE MILENIA*

**9. Kutatokea nini kwa Shetani? Ufunuo 20:1-3.**

*Shetani atafungwa kwa miaka ________________________________________.*

*Hatafungwa kwa dhahiri bali atafungwa kwa mazingira ambayo hatakuwa na mtu wa kumdanganya maadamu waovu watakuwa wamekufa na wale wenye haki watakuwa mbinguni. Ndivyo kipindi hiki kitakavyokuwa kwa Shetani.*

**10. Dunia itakuwa kama nini katika ile miaka elfu moja? Yeremia 4:23-27.**

________________________________________________________________________

*Ni nini kitaifanya dunia kuwa ukiwa?*

- Yale mapigo saba yatakuwa yameharibu sana.
- Har Magedoni itawaacha wengi kuwa wafu. Yeremia 25:33; Isaya 24:22.
- Lile tetemeko kuu la nchi la pigo la saba litaharibu miji mikuu yote ya dunia.
- Ujio wa Kristo kati ya miale ya moto utakamilisha maangamizi. 2 Wathesalonike 1:7, 8.

**11. Je, wale watakatifu (waliokombolewa) watafanya nini kule mbinguni? Ufunuo 20:4.**

________________________________________________________________________

- Watatathmini adhabu ambazo zinawastahili wale waovu. 1 Wakorintho 6:2, 3.
- Haki ya Mungu itadhihirika kwa njia ya kushiriki kwa watakatifu hawa katika hukumu.

## *MATUKIO MWISHONI MWA ILE MILENIA*

**12. Yesu atakuja katika dunia hii baada ya ile miaka elfu. Ni nani watakaoambatana Naye? Zekaria 14:4-6.** ________________________________________________

*Toleo la Straubinger linasema, "Katika siku ile hapatakuwa na nuru, ni baridi pekee pamoja na theluji." Zekaria 14:6.*

**13. Mtume Yohana aliona nini kikishuka kutoka mbinguni? Ufunuo 21:2.**

________________________________________________________________________

**14. Je, kutatokea nini kwa wengine waliokufa (waovu)? Ufunuo 20:5.** ________________

**15. Kutatokea nini kwa Shetani? Ufunuo 20:7.** *Ata________________ kutoka katika gereza lake.*

a) Mazingira yale yaliyomfanya kuwa mfungwa yatakuwa yametoweka, kadiri vile kutakuwako na watu wa kuwadanganya.

# 18 KITABU CHA UFUNUO NA HATIMA YA SAYARI YETU



Kutatokea nini juu ya sayari yetu hii katika mwisho wa dunia? Je, itatoweka? Kutatokea nini baada ya hilo? Sisi tutaishi wapi-kule mbinguni ama hapa duniani? Mungu aliiumba dunia hii ili ikaliwe na watu, lakini Paulo aliandika ya kwamba tutanyakuliwa mawinguni kwenda mbinguni (1 Wathesalonike 4:16, 17). Je, tutakuja kurudi tena duniani? Je, ni lini ambapo ile hukumu ya mwisho itakapofanyika na kutatokea nini kwa wale waovu? Je, watakuja kuadhibiwa? Kitabu cha Ufunuo kinasimulia juu ya vita dunia yote; hii itakuja kutokea wapi? Pia kinataja juu ya ile milenia, nayo ina mambo gani? Naye Shetani atakuwa wapi?

## MWENDELEZO WA MATUKIO

**1. Hivi leo yawezekana kuokoka. Tunaishi katika kipindi cha rehema. Je, ni kwa rai gani ambapo Mungu anawaambia wanadamu? Ufunuo 14:6, 7.**

______________________________________________

*Katika Ufunuo 18:4, anatutaka tutoke katika Babeli ambayo inawakilisha yale machafuko ya kiroho ya wakati wetu huu.*

**2. Mara ule mlango wa rehema utafunga. Fursa zote za kuchagua njia ya Mungu zitafikia mwisho, Naye Kristo ataacha kufanya uombezi kwa ajili ya wanadamu. Ndipo kutasikika nini kutoka mbinguni? Ufunuo 22:11.**

*"Mwenye kudhulumu na azidi ________________, …na mwenye haki na azidi ______________ ."*
Kwa maneno mengine, hatima ya kila mtu itakuwa imetiwa muhuri, kwa ajili ya wokovu ama kwa kupotea.

**3. Je, kutatokea nini baada ya kipindi cha rehema kwisha? Danieli 12:1; Ufunuo 15:1.**

*Wakati wa ___________________, kumaanisha ___________________ mapigo ya mwisho.*

**4. Jina la ile vita ya kutisha itakayotokea katika lile pigo la sita ni lipi? Ufunuo 16:16.**

______________________________________________

a) Mahali itakapopangiwa vita hii itakuwa ni katika Mashariki ya Kati, jirani na Yerusalemu.
b) Mataifa yote ya dunia yatahusishwa (Yoeli 3:9 -14).
c) Kutakuwako na umwagaji mkubwa wa damu (Ufunuo 14:20).
d) Vita hii itakuwa pia itakuwa ni pambano kati ya Shetani pamoja na wafuasi wake dhidi ya Kristo na watu Wake.
e) Ni nani atakayeshinda katika vita hii? Kristo atakuwa ni mshindi mkuu (Ufunuo 19:13-16).

## MATUKIO MWANZONI MWA ILE MILENIA

**5. Je, ni tukio lipi litakaloashiria mwisho wa dunia na mwanzo wa kile kipindi cha miaka elfu moja? Ufunuo 14:14-16.**

*__________________________ wa pili wa ______________________________.*

- Kila jicho litamwona (Ufunuo 1:7), na kila sikio litamsikia (1 Wathesalonike 4:16).
- Mbingu itakunjwa kama ukurasa ukunjwavyo, na visiwa vitaondolewa kutoka mahali pake (Ufunuo 6:14).

**13. Amri ya kumi inakataza nini? Kutoka 20:17.**

______________________________________________

*Tamaa ni mtangulizi wa dhambi nyinginezo, kama vile wizi na uzinzi (Mika 2:2). Hii ilikuwa ndio dhambi ya kwanza ya Hawa (Mwanzo 3:6). Mungu anataka kutulinda na kutufanya kuwa na furaha kwa njia ya sheria Yake.*

## HITIMISHO

*Msingi wa sheria ya Mungu ni upendo. Zile amri nne za kwanza zinatuonesha jinsi ya kumpenda Mungu. zile sita za mwisho zinatuonesha namna ya kumpenda jirani yetu. Warumi 13:9.*

**14. Lakini, twawezaje kumtii Mungu iwapo tu wadhaifu sana? Wafilipi 2:13; 4:13.**

______________________________________________

**15. Je, tunaipata mbingu kwa njia ya matendo ya utiifu? Kusudi la sheria ya Mungu ni lipi? Warumi 3:20, 24.**

______________________________________________

*Hatuwezi kuipata mbingu kwa njia ya matendo yetu. Wokovu ni kipawa tusichostahili kutoka kwa Mungu. Maasi yetu ya zamani yanatuhukumu, lakini kusudi la ile sheria ni kutuonesha sisi dhambi zetu ili twende kwa Yesu na kumwomba atusamehe na atusaidie kuubadili utaratibu wa maisha yetu. Utii ni kielelezo cha upendo wetu kwa Mungu na kumkubali kwetu Yesu kama Bwana wetu. Yohana 14:15.*

**16. Laiti tukisema pamoja na Paulo, "Bwana, wataka nifanye nini?" (Matendo 9:6) na tumechagua kuzitii amri za Mungu, tutapokea nini?**

*a) Kumbukumbu 28:1, 2, 9, 13. ______________________________________________*
*b) Maombi yetu yatajibiwa (1 Yohana 3:22). Tutakuwa nayo amani ya rohoni (Isaya 48:18), hekima (Zaburi 119:104), afya (Kutoka 15:26), pamoja na maisha marefu (Kumbukumbu 4:40).*

Ili kupokea mibaraka hii yote iliyoahidiwa, je, unakubali kuzitii amri zote za ile Sheria Takatifu ya Mungu kutokana na kumpenda Yesu? Je, unapenda kumwomba Bwana akusaidie kuzishika kwa uaminifu?

***Uamuzi wangu:** Nataka Mungu anijalie uwezo wa kushika kila moja ya hizi Amri Kumi, kwa njia ya imani.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

Mada inayofuata: *Kioo na Kivuli*




**12. Je, vile vitabu vya uganga pamoja na vitu vingine vya jinsi hii vifanyiwe nini? Matendo 19:19.**

______________________________________________

**13. Je, ni ushauri gani wa kimbingu ambao utatuweka huru kutokana na ile mivuto ya kishetani? Yakobo 4:7.**

*a)* ______________________ *Mungu.*

*b)* *Kumpinga* ______________________ *. Kutomsikiliza wala kumwamini.*

*c)* *Shetani* ______________________ *.*

**14. Je, tutumainie nini ili kupata ushindi kamili? Ufunuo 12:10, 11.**

______________________________________________

## *HITIMISHO*

- Pale Adamu na Hawa walipojitenga na Mungu, waliahidiwa ya kwamba Kristo atamshinda Shetani na kumponda kichwa chake (Mwanzo 3:15). Jambo hili lilitokea pale katika kifo cha Yesu.
- Yesu anataka kukutetea, kukusaidia, kukusamehe, na kukuficha wewe katika mikono Yake yenye upendo.

**15. Baada ya kumweka huru yule Mgerasi (Luka 8:26 -28), je, ni ushauri gani ambao Yesu alimpatia? Luka 8:38 39.**

______________________________________________

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba tunapasa kutafuta msaada kutoka kwa Yesu; sio kwa waonaji, waponyaji, wanajimu ama watu wa rohoroho.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

*HALAIKI YA PEPO*

**6. Ishara ya siku za mwisho ni ipi? 1 Timotheo 4:1.**

______________________________________________________________

a) *Sio Wana-rohoroho wenye mfumo pekee ndio waliopo, bali pia kuna wachawi na waaguaji; hawa pia wamejipenyeza katika makanisa ya Kikristo.*

b) *Kiti wa kwanza aliyepata kutumiwa alikuwa ni nyoka (Mwanzo 3:1-4). Viti wengine ni watu wengine ambao huingia katika hali kama ya usingizi mzito na kisha wale pepo huongea kwa kupitia kwao. Wanajifanya kuwa wanaweza kuwafanya wafu waongee, kuvisogeza vitu pasipo kuvigusa, kuponya wagonjwa, kutoa ujumbe, n.k.*

**7. Twawezaje kusema ukweli kutoka kwenye makosa? Isaya 8:19, 20.**

*Mjumbe wa Mungu ataafikiana na __________________ na _________________ katika kila jambo; ni lazima akubaliane na kile ambacho Mungu amekithibitisha huko nyuma kupitia kwa neno Lake.*

**8. Je, Biblia inasema nini juu ya wale wanaotafuta ufumbuzi wa matatizo yao kutoka katika nguvu hizo za giza? Yeremia 2:13.**

______________________________________________________________

a) Kwa misemo ya siku hizi, tunazungumza juu ya Parapsychology. Kuna watu ambao hupita kati ya moto bila ya kuungua nao husema ya kwamba wanaweza kufanya hivyo kutokana na nguvu za kiakili. Jambo hili Mungu alililikataza (Kumbukumbun18:9-14).

b) Kusoma viganja ni kuagua.

c) Kumtia mtu usingizi na kumwamrisha kimazingara, pamoja na kuponya kwa njia ya maneno ya kiganja, hata kama imefanywa kwa nia njema, Mungu hajazikubali.

**9. Je, Biblia inasemaje juu ya wale wanaofanya falaki na kuwauliza wanajimu? Isaya 47:13-15.**

______________________________________________________________

**10. Katika siku za mwisho, miujiza ya uongo itakuwa udanganyifu ambao utawapoteza hata ___________________________. Mathayo 24:24.**

*Kuna mambo ambayo pengine huwezi kuyaona kuwa ni mabaya sana, lakini yanaweza kuvifikia viwango vya yale Mungu asiyoyapenda; na hata kama huwezi kuliamini hili, wewe unaongozwa na nguvu fulani zilizofichika. Ni jambo bora zaidi kuachana na mambo yote ya jinsi hii.*

**11. Je, Shetani hutenda kazi yake bure, ama kama anatoza kwa ajili ya "hisani" zake? Warumi 6:16; Yohana 8:44.**

______________________________________________________________

*Shetani hulipisha kwa bei kubwa kwa wale wanaomwendea ili kushauriwa naye. Mtu huyo aweza kuletewa:*

- *Kutokuamini, mashaka, kupoteza imani juu ya neno la Mungu pamoja na sala.*
- *Msongo, wasiwasi, na hata kujaribu kujiua.*
- *Magonjwa ya kiakili, kuchanganyikiwa kiakili,*
- *Mapotofu ya kijinsia, uzinzi, ulevi, ughaibu wa madawa ya kulevya.*
- *Hasira isiyotawalika. Kupagawa na mapepo. Magonjwa, umaskini, nakadhalika.*

*Baada ya kuomba msamaha wa Mungu kwa ajili ya kushauriana na watu kama hawa ama kwa kutafuta usaidizi kutoka kwa watu mbalimbali zaidi ya Mungu, amua sasa kutofanya hivyo tena.*

# 12a KIOO NA KIVULI



Je, kuna ukinzani katika Biblia? Wala HAKUNA, hata kama yaweza kuonekana hivyo.

Kwa mfano, Yesu Kristo alizungumza kwa kukubaliana ile sheria katika Luka 16:17, na vivyo hivyo ndivyo alivyofanya Mtume Paulo katika Warumi 7:7, 12. Licha ya hili, yaonekana kwamba mtume yule yule anasema kinyume na ile sheria katika Wagalatia 3:10,13. Je, anajipinga mwenyewe?

Pale Mungu alipomwumba mwanadamu, aliweka kanuni za sheria Yake moyoni mwake (Mwanzo 2:16,17). ("usi………").

Mwanadamu, aliyeumbwa akiwa mwenye utashi, aliiasi ile sheria naye akafukuzwa kutoka Edeni (Mwanzo3:24). Mwanadamu alipasa kufa kwa ajili ya dhambi yake, lakini Mungu, kwa rehema Yake, akaweka wa mbadala kwa muda, mwanakondoo, ambaye alikuwa ni mfano wa Kristo, Mwokozi wa wanadamu. Zile ngozi kutoka kwa wale wanyama wa kwanza waliouawa ziliwapatia wanadamu mavazi (Mwanzo 3:21).

Kafara ya Habili ilikubaliwa. Alitoa mwana kondoo, ambapo kaka yake alileta matunda ya nchi naye akakataliwa na Mungu (Mwanzo 4:3, 4). Ili kusamehewa, mwenye dhambi alipaswa kuleta mnyama hekaluni, akaweka mikono yake juu ya kichwa cha yule mnyama, na kumtoa kafara. Hii iliashiria kwamba dhambi zake zilihamishiwa kwa yule mnyama, ambaye alikufa mahali pake (Walawi 4:27-29). Desturi hizi zote pamoja na maadhimisho, yalikuwa ni kivuli ama mfano ulioelekeza kwa Kristo. Kwa sababu hii, inaitwa kuwa ni Sheria ya Maadhimisho (Waebrania 10:1).

**1. Kuna aina ngapi za sheria?**

*Kando ya sheria za kijamii katika Israeli, Biblia inaeleza juu ya sheria nyingine mbili:*

a) Amri Kumi, ambazo zaweza kulinganishwa na kioo kinachotuonesha sisi juu ya hali yetu ya dhambi.

b) Sheria ya maadhimisho, ambayo inajumuisha pamoja na kafara, maadhimisho na sikukuu, ambazo zilikuwa ni kivuli ama mfano wa Kristo pamoja na kazi yake kwa mwanadamu.

Sheria hii alipewa mwanadamu baada ya anguko lake nayo ilikuwa ni njia ya ukombozi wake hata pale Mwana wa Mungu alipokuja na kufa katika dunia hii, mahali petu.

*Sheria hii alipewa mwanadamu baada ya anguko lake nayo ilikuwa ni njia ya ukombozi wake hata pale Mwana wa Mungu alipokuja na kufa katika dunia hii, mahali petu.*

**2. Je, kuna tofauti zipi kati ya sheria hizi mbili?**

*Katika jedwali ukurasa ufuatao, tutazilinganisha sheria hizo mbili (iangalie hivi sasa).*

**3. Je, ni kwa nini zile Amri Kumi hazikubatilishwa baada ya kifo cha Kristo?**

*Katika Agano la Kale na Agano Jipya, kile kioo cha sheria takatifu ya Mungu ilikuwa ni muhimu ili kwamba mwanadamu aweze kuitambua dhambi. Kilichobadili ilikuwa ni njia ambavyo msamaha ulivyopatikana. Katika Agano la Kale, mwana kondoo, ambaye alichukua mahali mwenye dhambi na kuelekeza mbele kwa Kristo, alipasa kutolewa kafara, ambapo katika Agano Jipya, pale tunapoziona dhambi zetu kulingana na ile sheria, tunaenda moja kwa moja kwa Kristo kwa njia ya imani. Pale Mwokozi alipokuja, ile sheria ya maadhimisho iliyomwakilisha Yeye haikuwa tena na umuhimu.*

**4. Je, Paulo anasemaje juu ya kutahiriwa? Je, hii nayo ilikuwa ni sehemu ya ile sheria ya maadhimisho? 1 Wakorintho 7:19.**

______________________________________________________________

Elimu inatuambia ya kwamba kuna faida pale tunapoishi kwa kulingana na mpango wa maadili ya milele, kwani ahadi za Mungu ni kwa ajili ya wale wanaoishika sheria Yake. Kumbukumbu 5:29; Zaburi 119:165.

| *AMRI KUMI* | *SHERIA YA MAADHIMISHO* |
|---|---|
| **1. Zinaitwa kama SHERIA YA MUNGU (Warumi 7:22)** | **1. Inaitwa kama sheria ya Musa (Matendo 15:5).** |
| **2. Ilitolewa tokea Edeni (Warumi 2:15)** | **2. Ilitolewa baada ya Edeni (Wagalatia 3:19)** |
| **3. Iliandikwa kwa chanda cha Mungu (Kutoka 31:18).** | **3. Iliandikwa na Musa (Kumbukumbu 31:24).** |
| **4. Ziliandikwa juu ya mawe (kitu imara).** | **4. Ni kitabu.** |
| **5. Ziliwekwa ndani ya Sanduku la Agano, mahali patakatifu zaidi, ambayo ni ishara ya kiti cha enzi cha Mungu (Kumbukumbu 10:1-5).** | **5. Iliwekwa kando ya Sanduku la Agano (Kumbukumbu 31:25, 26).** |
| **6. Sheria inafananishwa na kioo; inatuonesha hali yetu ya dhambi (Warumi 7:7).** | **6. Sheria ya maadhimisho ilikuwa kwa ajili ya upatanisho ama msamaha wa dhambi (Waebrania 9:22).** |
| **7. Ilikuwa ni njia ya maisha ambayo tunapasa Kuishi kwa hiyo (1 Timotheo 1:8-10).** | **7. Ilikuwa tu ni ishara inayotuelekeza kwa Kristo (Waebrania 9:9).** |
| **8. Ni za milele, Kristo hakuzibatilisha (Zaburi 111:7, 8; Mathayo 5:17).** | **8. Ilibatilishwa na Kristo (Wakolosai 2:14).** |
| **9. Unabii ulisema ya kwamba Yesu angeiadhimisha sheria (Isaya 42:21).** | **9. Paulo asema wazi ya kwamba Yesu aliibatilisha sheria ya maadhimisho (Waefeso 2:15).** |
| **10. Yule anayeishika sheria ya Mungu anaitwa kuwa aliyebarikiwa (Yakobo 1:25).** | **10. Yule anayeyashika yale yaliyoandikwa katika kitabu cha sheria anaitwa kuwa aliyelaaniwa. Baada ya kifo cha Kristo, hapana haja ya desturi hizi (Wagalatia 3:10-13).** |
| **11. Tutahukumiwa kwa sheria (Yakobo 2:10-12).** | **11. Tusihukumiwe kwa kile tulacho, tunywacho, Sikukuu (Sabato za maadhimisho n.k.) ambazo zilikuwa ni kivuli cha yale yatakayokuja (Wagalatia 2:16, 17).** |
| **12. Twaweza kuzishika zile Amri Kumi kwa msaada wa Mungu (1 Yohana 5:3).** | **12. Sheria ya Musa haikuwezekana kuishika (Matendo 15:10).** |

***Uamuzi wangu:*** *Ninakubali ya kwamba zile Amri Kumi, sheria ya Mungu; na ile sheria ya Musa, ambayo ni sheria ya maadhimisho, ni sheria mbili zilizo tofauti. Ile ya kwanza ni ya milele na ile ya pili ni ya kitambo.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

# 17 USHAURI WA KIMBINGU DHIDI YA NGUVU ZA GIZA



Dunia hii tunayoishi imejaa mambo mengi ya nguvu za giza ambayo yanatufanya sisi kushangaa sana. Kuna watu ambao huzungumza na wafu, nguvu fulani zisizo za kawaida ambazo zinaweza kutenda mema ama mabaya, kama vile kuponya kimujiza, n.k. Kuna mikutano ya rohoroho ambapo wale kina kiti hupagawa na pepo; vipande vya samani hurushwa huku na kule. Kuna nyumba fulani ambazo kwa halisi hupenda kutembelewa, ambamo taa fulani huwashwa na sauti fulani za kigeni husikika kunako usiku wa manane, n.k. Kuna nguvu fulani za giza zilizowaleta watu kwenye mashaka, magonjwa na kutengana na familia, na kifo. Hata wanasiasa, wafanya biashara pamoja na watu maarufu huwaendea wale wapiga ramli. Mamilioni ya watu husoma maaguzi kwa nyota kwa kila siku, wengine wanasomewa kadi zao, lakini hawa wote hudanganywa tu. Nguvu hizi za giza hutoka wapi? Tunawezaje kulindwa dhidi ya nguvu hizo? Mungu ndiye pekee ajuaye kama kuna nini huko mbele. Ameyafunua haya katika nabii za Biblia zipatazo 2,300. Wapiga ramli wanayajua ya wakati huu na ya wakati uliopita, na jambo hili huwaingia watu moyoni; hii ni kwa sababu wanafanya kazi pamoja na pepo ambao sisi hatuwezi kuwaona, lakini hata hivyo wako upande wetu. Hawa ni pepo wale wale wanaotokea katika mikutano ya rohoroho. Isaya 8:19.

### *NGUVU HIZI ZA AJABU NI NANI?*

**1. Je, hizi zitakuwa ni roho za wafu? Biblia inasemaje juu yao waliokufa? Mhubiri 9:5, 6.**

________________________________________

**2. Je, yawezekana kwamba Mungu ndiye anayewaongoza hawa? Ni amri gani Mungu aliyotoa? Walawi 20:27; Kumbukumbu 18:10-12.**

________________________________________

**3. Iwapo mafunuo haya hayaji kutoka kwa Mungu wala kwao waliokufa, ni nani anayewahamasisha wanasiasa? Ufunuo 16:14.**

________________________________________

a) Roho hizi za mapepo ni wale malaika walioanguka ambao walimwasi Mungu (Ezekieli 28:13-18).
b) Theluthi moja ya malaika walifukuzwa kutoka mbinguni (Ufunuo 12:9, 12).

**4. Katika mifano ya Kibiblia juu watu waliopagawa na pepo, wale pepo walisema nini bayana? Matendo 16:16-18. Weka alama katika jibu sahihi:**

❑ Walisema uongo

❑ Walisema mambo yasiyo na maana

❑ Mlikuwamo na ukweli katika yale waliyoyasema.

**5. Kulitokea nini kwa Mfalme Sauli pale alipokwenda kwa wapiga ramli baada ya Mungu kumkataa? 1 Samweli 28:3, 6 - 8, 11-15; 1 Nyakati 10:13, 14.**

________________________________________

*Kwa miaka 6,000, Shetani amehubiri uongo huu, ambao umeaminiwa na karibu ya waungwana wengi. Desturi za ibada za wafu zilikuwapo miongoni mwa Wamisri, ambao waliweka samani, vyakula, hazina za thamani ndani ya makaburi ya Mafarao. Kuna mamilioni hivi leo ambao huamini ya kwamba wale wafu wanafurahia uzima wa milele ama wanateseka na adhabu kule kuzimu ama purgatori.*

**13. Je, ni nani pekee asiyefikwa na umauti? 1 Timotheo 6:15, 16.**

______________________________________________

*Yesu anataka kuwapatia hali ya kutofikwa na umauti watoto Wake, pale ajapo mara ya pili. 1 Wakorintho 15:51-55.*

**14. Je, tunayo tayari hali ya kutokufa, ama tunaitafuta? Warumi 2:7.**

______________________________________________

## *HITIMISHO*

Kifo ni kinyume cha uzima. Pale mtu afapo, anakoma kuwapo; anakuwa hana ufahamu. Licha ya hili, tumaini letu kubwa liko katika kuja kwa mara pili kwa Yesu, pale tutakapokutana na wapendwa wetu waliokufa katika Kristo.

**15. Hatimaye Yesu atafanya nini na kifo? Ufunuo 21:4.**

______________________________________________

Daima tunapasa kujitayarisha kwa sababu maisha yetu yananing'inia kama kwa uzi.

*__Uamuzi wangu:__ Ninaamini ya kwamba wafu hawajui kitu cho chote, nao wanalala hata ule ufufuo wa mwisho.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

# 13 NJIA BORA ZAIDI YA KUUSHINDA MSONGO



Hivi leo tunaishi chini ya msongo, unyong'onyevu, na fadhaa, ambazo huathiri afya na furaha yetu. Asilimia 70 hadi 90 ya magonjwa yote ni ya kiakili, kama matokeo ya fadhaa zetu. Tunahitaji pumziko la kimwili na kiroho, ili kuyajua sana mambo ya nafsi yetu ya ndani pamoja na kufahamiana na Muumba wetu, ambaye wengi wetu tumempuuzia ama hata kumkataa. Tunapouchunguza uumbaji, tunashangaa. Chukulia kwa mfano, kuzaliwa kwa mtoto, kiumbe awezaye kuona, kusikia, kujisogeza, na kutoa sauti. Akili za mwanadamu, pamoja na uwezo wake mwingi wa kutafakari; jicho lilivyo na utendaji wake wa kustaajabisha; na pale tunapoziangalia nyota katika anga la juu, ama unapowaangalia viumbe walio wadogo sana, uyaangalie yale maua mazuri ya kupendeza bustanini, mwangalie mchanga akitabasamu, hatuna jingine isipokuwa kumtukuza Mungu. Zaburi 139:13, 14.

## *HEBU NA TUMTUKUZE MUUMBA!*

**1. Je, Mungu anastahili nini kwa ajili ya yale aliyoyaumba? Ufunuo 4:11.**

______________________________________________

**2. Je, Mungu alihitaji maelefu ya miaka ili kuiumba dunia? Ilimchukua muda gani? Mwanzo 1:31.**

______________________________________________

- *Katika siku ya kwanza, Mungu aliumba nuru (Mwanzo 1:1-5). Dunia ilikuwa tupu na ukiwa.*
- *Katika siku ya pili, aliumba anga na mbingu (mstari wa 6-8).*
- *Katika siku ya tatu, aliumba nchi na mimea (mstari wa 9-13).*
- *Katika siku ya nne, alipangilia mfumo wa anga (jua, mwezi, na nyota (mstari wa 14-19).*
- *Katika siku ya tano, aliumba samaki na ndege (mstari wa 20-23).*
- *Katika siku ya sita, aliumba wanyama wa nchi pamoja na mwanadamu (mstari wa 24-28, 31).*

**3. Je, alifanya nini panapo siku ya saba? Mwanzo 2:1-3.**

*Mungu* ______________________________ *siku ya saba.*

a) Mungu hakupumzika kwa sababu amechoka bali kutupatia sisi kielelezo.

b) Mungu hakibatilishi kile alichokibariki na kukitakasa. Hesabu 23:19, 20.

*Minara (sanamu) ya kumbukumbu imejengwa mara nyingi ili kuwaheshimu watu wakubwa, kama vile wapiganiauhuru, mashujaa, washairi, wavumbuzi, walimu, kinamama, watu walioitumikia jamii ama kuokoa maisha. Kule Bern, Uswisi kuna kumbukumbu ya mtakatifu Bernard aliyewaokoa watu 14 katika milima ya Alps.*

**4. Je, ni kumbukumbu gani iliyowekwa katika amri ya nne ya Sheria Takatifu ya Mungu ili kumheshimu Yeye kama Muumba? Kutoka 20:8-11.** ______________________

## *KUITUNZA SIKU YOTE YA SABATO*

**5. Je, Mungu anaionje Sabato? Ezekieli 20:12, 20.** ______________________

*Muhuri ina vipingee vitatu: 1. Jina, 2. Cheo, 3. Eneo la mamlaka. Katika ile amri ya nne (Kutoka 20:8-11) tunavikuta vipengee hivi ifuatavyo:*

**1. Jina:** Bwana Mungu wako. **2. Cheo:** Muumba (Mungu aliumba…..). **3. Eneo la mamlaka:** Mbingu na nchi.

**6. Je, Sabato ilipata kuadhimishwa kabla ya kutolewa kwa ile sheria katika Mlima Sinai? Kutoka 16:15, 21 -30.** ______________________

*Uthibitisho wa jambo hili ni muujiza wa ______________________. Tangia pale, utaratibu wa juma haujapata kubadilishwa katika kalenda ya Wayahudi wa kale, wala katika kalenda yetu sisi wenyewe.*

**7. Je, Isaya ameielezeaje siku ya Sabato? Isaya 58:13, 14. ________________________**

**8. Je, hii Sabato iliwahusu waumini wasio Wayahudi wa Agano la Kale na Wakristo wa leo pia? Isaya 56:2-7. ________________________________________________**

## *JE, YESU NA WANAFUNZI WAKE WALITUNZA SABATO?*

**9. Uhusiano wa Yesu na Sabato ukoje?**

*a) Kristo Mwenyewe ndiye aliyeiumba. Yohana 1:1-14; Wakolosai 1:15-17.*
*b) Aliitangaza ile sheria katika Mlima Sinai. Nehemia 9:12, 13; 1 Wakorintho 10:4.*

**10. Je, desturi ya Yesu ilikuwaje pale alipokuwapo hapa duniani? Luka 4:16, 31.**

________________________________________________

**11. Je, Sabato ilifanywa kwa ajili ya watu wote? Marko 2:27, 28. ____________________**

*a) Yeye ndiye Bwana, Mmiliki na Mwanzilishi wa Sabato, kwa hiyo ni siku ya Bwana.*
*b) Alifundisha jinsi ya kuitunza kwa kutenda mema na kuhubiri panapo siku hii. Mathayo 12:27, 28.*

**12. Je, Mariamu mama yake Yesu pamoja na wanawake wengine waaminifu waliofundishwa na Yesu, walifanya nini baada ya kusulubiwa Kwake? Luka 23:56.**

________________________________________________

**13. Je, Sabato ingeendelea kuwa takatifu hata baada kifo cha Kristo? Ni ushauri gani aliowapatia wanafunzi Wake pale alipowaelezea juu ya kuangamizwa kwa Yerusalemu, jambo ambalo lilitokea zaidi ya miaka 40 baadaye (mwaka 70 B.K.)? Mathayo 24:20.**

________________________________________________

**14. Je, mitume nao walitunza Sabato?**

a) Kule Korintho. Matendo 18:3, 4.
b) Kule Thesalonike. Matendo 17:2, 3.
c) Kule Antiokia. Matendo 13:14, 42, 44.
d) Kule Filipi, kando ya mto. Matendo 16:13.

**15. Je, ni wapi ambako Sabato itatunzwa milele? Isaya 6:22, 23. ____________________**

- Yesu alieleza ya kwamba Sabato ilifanywa kwa ajili ya kumfaidia mwanadamu. Marko 2:27.
- Ni njia bora zaidi ya kuushinda msongo pamoja na unyong'onyevu. Inatupatia pumziko la mwili, nafsi na roho.
- Ni siku ya kuwasiliana na Yesu pale tunapokutanika pamoja, kama vile alivyofanya Yeye. Hivyo, tunaimarisha uhusiano wetu pamoja Naye, nasi tunafunguka kutoka katika msongo wa kisaiklojia na kupata pumziko na amani ya nafsi yetu. Mathayo 11:28-30.
- Tunamheshimu Muumba wa uhai pale tunapofurahia mambo ya asili na kumpatia heshima, utukufu na uweza wa kuumba kila kitu.
- Ni siku ya kuiweka wakfu familia na kuwafundisha watoto wetu juu ya njia za Mungu.

**16. Je, yawezekanaje kuitunza siku hii takatifu katika dunia iliyopinduka juu chini? Wafilipi 4:13; Zaburi 37:3-5; Isaya 65:13. ________________________________**

*Tunapata furaha pale tunapoonyesha upendo wetu kwa Mungu! Tutapata dhamira iliyotakata pamoja na uhakika wa kukamilika kwa wajibu wetu.*

*__Uamuzi wangu:__ Ninaamini ya kwamba Sabato ni siku sahihi ya kupumzika nami ninapenda kuitunza.*

❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

***Kitu (udongo) – pumzi ya uhai = kifo.** Kama ilivyo katika jambo la taa, udongo unakuwa hauwezi cho chote pale Mungu anapoondoa ile pumzi ya uhai.*

## *JE, KIFO NI KUWA KATIKA HALI YA UFAHAMU?*

**3. Je, wafu wanafahamu kitu cho chote? Mhubiri 9:5.**

________________________________________________

**4. Kunatokea nini juu ya hisia zao? Mhubiri 9:6, 10.**

________________________________________________

**5. Je, wafu wako katika hali ya ufahamu wo wote? Zaburi 146:4.**

________________________________________________

**6. Je, wafu wanajua lo lote juu ya jamaa zao? Ayubu 14:21.**

________________________________________________

**7. Je, wako mbinguni wakimsifu Mungu? Zaburi 115:17; Isaya 38:18, 19.**

________________________________________________

## *KIFO KINAFANANISHWA NA NINI?*

**8. Je, Yesu anakifananisha kifo na nini? Yohana 11:11 -14.**

________________________________________________

*Ayubu naye anakifananisha kifo na usingizi. Wafu wamelala; hawana ufahamu wo wote hadi pale watakapoamka katika ule ufufuo. Ayubu 14:10-12.*

**9. Je, ni mfano gani mwingine ambao Maandiko hutupatia? Ayubu 14:1, 2.**

________________________________________________

## *JE, TUTAWAONA TENA WALE WALIOKUFA?*

**10. Je, tumaini lenye utukufu la wale walikufa wakimwamini Mungu ni lipi? Isaya 26:19; 1 Wathesalonike 4:14-17.**

________________________________________________

**11. Je, wale waaminifu wa kale waliokufa tayari wanafurahia uzima wa milele? Waebrania 11:39, 40; Danieli 12:13.**

________________________________________________

*Kuna mkanganyiko kati ya wale wanaohubiri ya kwamba kuadhibiwa ama kuzawadiwa hufanyika mara moja, na wakati huo huo wanahubiri juu ya ufufuo na ile hukumu. Iwapo mtu anapoikea tuzo yake pale anapokufa, ni kwa nini basi Yesu aje kuwahukumu wafu na walio hai? Atahukumu nini? Je, ni kipi kilichopokelewa tayari?*

## *UDANGANYIFU MKUBWA, NA MKONGWE ZAIDI ULIOWADANGANYA MAMILIONI*

**12. Mungu aliwaambia Adamu na Hawa ya kwamba kama wangekosa kutii wangekufa (Mwanzo 2:16, 17). Hata hivyo, uongo mkubwa wa Shetani ulikuwa ni nini? Mwanzo 3:4.**

________________________________________________

# 16 JE, KUNA MAISHA BAADA YA KIFO?



Mara nyingi, tunashangaa kwamba kunatokea nini baada ya kifo. Kuna wale ambao, baada ya tukio wamehuishwa na kueleza juu ya mambo waliyoyafahamu kwenye kifo. Mara nyingi tunasikia ya kwamba waliokufa wamejidhihirisha wenyewe; wengine hata kuongea nao.

Je, inafaa kuogopa kifo?

Mara kwa mara tumekutana na kifo ana kwa ana; tunapohudhuria mazishi ya rafiki ama ndugu kwenye kumuaga, ama pale tunapoliona lile gari la kuchukua maiti mazikoni likifuatiwa na waombolezaji waliovalia mavazi meusi. Tunashangaa, kuna maisha baada ya kifo? Pengine pale tunapoweka mashada ya mauwa juu kaburi tunajiuliza wenyewe, je, wafu wanao ufahamu wo wote?

Mke, akiwa amevunjika moyo kutokana na uchungu na kububujikwa na machozi, anashangaa, hivi nitakuja kumwona tena?

Kuna maoni mbalimbali juu ya jambo hili. Wengine wanasema ya kwamba mtu anapokufa huenda moja kwa moja mbinguni, purgatori ama kuzimu; wengine wanaamini ya kwamba amekwenda kwenye ulimwengu wa roho ama anafanyika upya na kuzaliwa kuwa kiumbe kipya; wengine bado wanasema ya kwamba hapa yote yamefikia mwisho wake; wengine wanasema ya kwamba mtu aliyekufa hafahamu kitu cho chote hadi siku ile ya ufufuo. Ni nani aliye sahihi? Kwani Mungu amesemaje? Biblia inatupatia jibu gani? Ayubu 14:14.

## MCHAKATO WA UHAI NA KIFO

**1. Ili kuufahamu mchakato wa kifo, kwanza na tutafakari kama ni jinsi gani uhai ulivyoanza? Mwanzo 2:7.**

____________________________________________________________

*Mwanadamu amefanyizwa kwa vitu viwili. Mungu alichukua kitu cha kwanza kutoka katika mavumbi ya ardhi. Mwili wa mwanadamu umefanyizwa kwa protini, mafuta, madini (kama vile fosforasi, chuma, magnesia, kalshamu, n.k.), na asilimia kubwa ni maji. Kiasi cha thamani halisi ya vitu hivi si zaidi kuliko $5; hii ndio thamani ya vitu vya mwili wetu. Tungekuwa na thamani ndogo kiasi gani kama isingekuwa ni pumzi ya uhai ya Mungu! Muunganiko wa vitu hivi viwili ndivyo vilivyomfanya mwanadamu, kiumbe kipya kabisa.*

a) Kama tungelifafanua jambo hili kwa mlinganisho wa kihisabati tungesema:
**kitu (udongo) + pumzi ya uhai = nafsi hai** (nafsi inayoishi).

b) Pale Mungu alipomwumba mwanadamu, mwanadamu akawa nafsi hai; haisemi ya kwamba Mungu alitoa nafsi ama kwamba mwanadamu anayo nafsi, bali munganiko wa mavumbi ya udongo na pumzi ya uhai ukamfanya yeye kuwa nafsi hai; kwa hiyo, mwanadamu ni nafsi. Pale tunaposema ya kwamba nafsi 3,000 walibatizwa, hatusemi kwamba roho 3,000 zilibatizwa bali ni watu.

c) Kuna mazao tofauti ya kikemikali ambayo, yanapochanganywa, huleta kitu kingine tofauti kabisa. Kwa mfano, ukichanganya atomi mbili za haidrojini pamoja na moja ya oksijini, tunapata maji, H20.

d) Iwapo taa ya umeme inapokea umeme, inatoa mwanga kutokana na mkondo wa umeme ulioifikia. Pale nishati hiyo inapozuiwa, ile nuru hutoweka. Ile taa haiwezi kutoa nuru yenyewe, wala umeme wenyewe hautoi nuru wenyewe.

**2. Maadamu mchakato wa kifo ni kinyume cha uhai, je, ni nini hutokea pale mtu anapokufa? Muhubiri 12:7; Zaburi 104:29.**

____________________________________________________________

# 14 UDANGANYIFU MBAYA ZAIDI KATIKA HISTORIA



Udanganyifu umetapakaa katika kila nyanja za jamii. Huu tunaukuta katika sayansi, katika uchumi wa sanaa, uandishi, na penginepo. Kwa bahati mbaya, pia kuna udanganyifu katika mambo ya kidini. Udanganyifu mbaya zaidi wa vizazi vyote ni ule wa desturi za kipagani za ibada ya mungu jua ambayo kwa ujanja imechomekwa katika Ukristo, kwenye kiwango cha kuingiza ibada ya jua badala ya ile ya zile Amri Kumi.

Ibada ya jua ni ya zamani kabisa. Mithras, Aurora, Marduk, Baal, Ra, Osiril na Shamas walikuwa ni miungu walioliwakilisha jua.

## IBADA YA JUA ILIYOGEUZWA

**1. Je, ni machukizo gani ambayo nabii Ezekieli aliyaona katika maono? Ezekieli 8:15-18.**

____________________________________________________________

Mungu alitamka hukumu kali kabisa juu ya waabudu jua (Ezekieli 6:4-6).

**2. Je, ni nani aliyejaribu kuleta desturi za kipagani katika Ukristo? Kwa nini?**

*Mfalme Konstantino (mwaka 280-337B.K.) aligundua ya kwamba nguvu za kisiasa za Rumi zilikuwa zinadhoofu kutokana na tofauti zilizokuwa zinajitokeza kati ya waabudu upagani na Wakristo. Ndipo akathubutu kuyaleta makundi haya mawili makubwa pamoja. Mnamo 313 B.K., alichapisha ile Sheria ya Milano, ambayo ndani yake alileta ustahimilivu wa kidini na uhuru kamili kwa Wakristo.*

*Matokeo yake, walionesha heshima kubwa kwa Mfalme huyu. Wapagani waliabudu miungu mingi, Mithraso akiwa ni mmoja wapo wa mungu jua wakuu.*

*Mathraso aliabudiwa panapo Jumapili. Hata leo, siku ya kwanza ya juma katika Kingereza ni Sunday, na katika Kijerumani ni Sonntag, yote yakimaanisha siku ya jua yanapofasiriwa.*

*Ili kuitimiliza agenda hii ya kisiasa, Konstantino mwenyewe akaingia katika Ukristo na akainzisha Jumapili, siku ya jua, kama siku ya kupumzika, badala ya Sabato iliyoadhimishwa na Wakristo waaminifu, jinsi hii alikidumisha kiunganishi pamoja na waabudu jua.*

*Wengi wakawa "Wakristo" na kuleta idadi kubwa ya desturi za kipagani katika Ukristo. Kadinali John Henry Newman katika kitabu chake "Development of Christian Doctrine" (Maendeleo ya Mafundisho ya Kikristo), uk. 373 anasema: "Eusabius anatueleza sisi ya kwamba Konstantino, anapoipendekeza dini hii mpya kwa wapagani hawa, akihamishia huko yale madoido ya nje ambayo wapagani hawa wameyazowea katika madhehebu zao; matumizi ya vihekalu vilivyowekwa wakfu kwa watakatifu maalumu, mapambo yalifanyizwa katika nyakati fulani kutokana na matawi ya miti, ubani, taa mbali mbali, mishumaa, sadaka za nadhiri kwa ajili ya kuponywa kwa wagonjwa, maji matakatifu, sikukuu za majira, matumizi ya kalenda, maandamano, kubariki mashamba, mavazi ya makuhani, pete za ndoa, desturi za kukabili mashariki, na baadaye sanamu za watakatifu, pengine na nyimbo za kikanisa na ile "Kyrie Eleison" (Bwana utuhurumie), desturi hizi zote zikiwa na asili yake katika upagani na zikiwa zimetakaswa pale zilipopokelewa na kanisa."*

*The Encyclopedia Britannica (toleo la 9) katika mada ya "Jumapili" inaeleza: "Kutambuliwa kwa awali zaidi kwa kuadhimishwa kwa Jumapili kama wajibu wa kisheria ni katiba ya Konstantino mnamo 321 B.K. (Machi 7) akieleza ya kwamba mahakama zote za sheria, wakazi wa mijini, pamoja na karakana zilipasa kuwa katika pumziko panapo Jumapili kukiwa na kuachiliwa kwa wale wnaojihusisha na kazi za kilimo."*

3. **Konstantantino alikuwa ni mfalme tu, sasa uadhimishaji wa Jumapili uliingizwaje ndani ya kanisa?**

*Badiliko la siku ya pumziko lilipokelewa na Kanisa la Roma. Katekisimo iliyopokea baraka za kitume za Papa Pius X (Januari 25, 1910) zikifafanua kama ifuatavyo:*

- Swali: Siku ya pumziko ni ipi?
- Jibu: Jumamosi ndio siku ya pumziko.
- Swali: Je, ni kwa nini tunaiadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi?
- Jibu: Tunaiadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki, katika Sinodi ya Laodikia (mwaka 336), lilihamisha yale maadhimisho kutoka Jumamosi kwenda Jumapili. Peter Geiermann, The Convert's Catechism of the Catholic Doctrine, (Katekisimo ya Waongofu wa Mafundisho ya Wakatoliki) 1964 uk. 50.

## *JE, MUNGU ANARUHUSU SHERIA YAKE KUBADILISHWA?*

4. **Je, kutatokea nini kwa ye yote anayethubutu kuibadili sheria ya Mungu? Ufunuo 22:19.**

_______________________________________________

5. **Je, ni kitu gani ambacho hakiruhusiwi kufanyika katika Sheria Takaifu ya Mungu? Muhubiri 3:14.**

_______________________________________________

a) Mungu hawezi kuibadili sheria Yake. Malaki 3:6; Yakobo 1:17.
b) Sheria ya Mungu itadumu kwa vizazi elfu. Kumbukumbu 7:9.
c) Ni kweli kwamba Amri Kumi ziliandikwa kwa kidole Chake Mungu Mwenyewe katika zile mbao mbili za mawe (Kutoka 20:8-11) ikionesha juu ya umuhimu na kutotanguka kwake.
d) Ile amri inayotueleza kwamba tuishike Sabato kama siku ya pumziko ni amri ya nne ya ile Sheria Takatifu. Kutoka 20:8-11.

6. **Je, Yesu aliibadili sheria ya Mungu ama siku ya kupumzika? Mathayo 5:17, 18.**

*Yesu alisema:* _______________________________________________

7. **Kwa kulingana na unabii wa Danieli, ile mamlaka ya kibinadamu ingejaribu kufanya nini juu ya sheria ya Mungu? Danieli 7:25.** _______________________

*Kanisa linaamini ya kwamba linayo mamlaka ya kufanya hivyo. Stephen Keenan, Kasisi Mkatoliki, aliandika: "Laiti kama (kanisa) lisingekuwa na mamlaka kama hayo, lisingeweza kufanya kile ambacho wanadini wote wa kisasa wanakubaliana naye; lisingeweza kubadili uadhimishaji wa Jumapili-siku ya kwanza ya juma, mahali pa kuiadhimisha Jumamosi-siku ya saba ya juma, badiliko ambalo halina mamlaka ya Kimaandiko." A Doctrinal Catechism, uk. 74.*

## *JE, MISTARI HII NANE INAYOITAJA SIKU YA KWANZA YA JUMA, INATAJA BADILIKO KATIKA ILE SIKU YA PUMZIKO?*

8. **Kwani mistari hii mitano kuhusu ule ufufuo, uliotokea siku ya kwanza y juma, inataja badiliko lo lote la siku ya kupumzika? Mathayo 28:1; Marko 16:1,2; 16:9; Luka 24:1; Yohana 20:1.**

_______________________________________________

9. **Je, ni kwa nini wale wanafunzi walikutanika siku ya kwanza ya juma? Yohana 20:19.**

*Ni kwa sababu walikuwa wanawaogopa* _______________________

*Ushahidi zaidi ya kwamba hawakukusanyika ili kuiadhimisha Jumapili kwa heshima ya kule kufufuka ni kuwa hata hawakuamini ya kwamba Kristo alifufuka. Marko 16:12-14.*

14. **Je, ni kitu gani ambacho hatuwezi kukisahau iwapo tunaongozwa na upendo? Yakobo 1:27.**

_______________________________________________

15. **Je, ni kitu gani ambacho hatuwezi kukipuuzia iwapo tunawapenda kiukweli jirani zetu? Marko 15:9; Zaburi 16:12-14.**

_______________________________________________

## *HITIMISHO*

Kupenda kunatufanya sisi kuwa na furaha! Tunabarikiwa zaidi tunapotoa kuliko kupokea (Matendo 20:35).

Upendo sio hisia pekee bali ni kanuni ya maisha. Upendo unatufanyna sisi kuwa wastahimilivu, wenye kusamehe, wanyenyekevu na waaminifu kwa Mungu pamoja na jirani zetu (1 Wakorintho 13).

Matokeo ya kuishi katika viwango hivi viwili kwa kila siku, tukimtii Mungu na sheria Yake, ni ufunguo wa mafanikio na furaha yetu (Kumbukumbu 28:1, 2).

Kristo amefanya kila kitu kwa ajili yangu. Nami nimpe kitu gani?

***Uamuzi wangu:** Ninakubali ya kwamba upendo wangu kwa Mungu pamoja na jirani yangu huonyeshwa katika kuzishika zile amri za ile Sheria Takatifu.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

*Kiroho:* *kufurahia lile badiliko Kristo alilolifanya ndani yetu. Haipasi kuwa ni pumziko la kimwili tu bali ni pumziko ambamo Kristo, Mwanzilishi na Bwana wa Sabato, anakuwa ni pumziko letu la kiroho kwa njia ya kazi Yake ya kutuhesabia haki (Waebrania 4:1, 2, 9, 10). Kila Sabato yapasa kuwa kionjo cha mbele cha uzima wa milele.*

**8. Sabato huanza na kwisha lini? Biblia inaiitaje ile siku ya sita?**

*a) Kwa kulingana na Biblia, siku huanza pale jua linapozama. Walawi 23:32; Nehemia 13:19.*
*b) Ijumaa, siku ya sita, inaitwa siku ya maandalio. Marko 15:19.*

***Kina mama wa nyumbani pia wastahili pumziko, hivyo wanapasa kufanya nini katika ile siku ya maandalio? Kutoka 16:23.*** *Maadamu ni siku halisi ya maandalio, tunapasa kununua kila kitu kinachohitajika, kusafisha nyumba, kuoga na kubadili nguo, na kuweka kando mavazi yatakayotumika Sabato.*

**9. Je, ni jinsi gani ambavyo Bwana anataka tuitunze ile anayoiita kuwa ni "Siku ya Utakatifu Wangu"? Isaya 58:13, 14.**

________________________________________

a) Kutofanya ________________________, yaani kutofanya biashara zo zote, ama kujitia wenyewe katika majukumu mbali mbali, pamoja na starehe, n.k.
b) Kutosafiri pasipo lazima isipokuwa katika kumtumikia Bwana.
c) Kuto________________________ juu ya matatizo ama vitu vinavyoonekana. Kutosoma magazeti ama kusikiliza habari. Inapasa kuwa ni siku takatifu hasa iliyowekwa kando kwa ajili ya Mungu.
d) Tusifanye mambo ambayo yatawafanya watu wengine watutendee sisi kazi (Kutoka 20:10).

**10. Iwapo tunampenda Mungu, ni majibu gani tutakayoyatoa kwenye vipingamizi vifuatayo?**

a) Kwani siku zote sio sawa? Kutoka 20:11; Mithali 16:25. Mungu alistarehe, akaitakasa na kuibariki siku hii maalumu.
b) Watu wengi huiadhimisha Jumapili. Je, mamilioni haya ya watu wanaweza kukosea? Mathayo 7:13, 14.
Suala husika sio kama tunasimama upande wa walio wengi ama walio wachache, bali ni iwapo tupo upande wa Yesu.
c) Wazazi wangu na kina babu walitunza Jumapili, nami sipendi kuwa tofauti. Matendo 17:30. Mungu husamehe dhambi zote zilizokwisha tendeka kutokana na kutofahamu (Yakobo 4:17).

**11. Iwapo tunampenda Yesu, tutafanya nini katika siku Yake? Luka 4:16.**

*Yesu alikuwa na desturi ya* ________________________________________

*a) Tunapasa kuhudhuria ibada za kidini ili kumwabudu na kusikiza neno Lake.*
*b) Twaweza kuwatembelea wagonjwa na kupoza maumivu yao (Mathayo 12:11, 12).*
*c) Twaweza kuongea na watu wengine juu ya habari njema ya wokovu.*

## *TWAWEZAJE KUPENDA KATIKA KIWANGO KILE KINGINE?*

**12. Zile amri sita za mwisho zinawahusu jirani zetu. Tunauoneshaje upendo wetu kwao?**

a) Amri ya tano inahusu mahusiano kati ya wazazi na watoto wao (Waefeso 6:1-4).
b) Iwapo ninampenda jirani yangu, naweza kumwua? Naweza kuchukua silaha vitani na kuua wingi wa watu? Naweza kutokuwa mwaminifu kwa mwenzi wangu? Je, naweza kusema mambo mabaya juu ya jirani yangu, uongo, kuiba, ama kutamani kitu chake (Warumi 13:9)?

**13. Iwapo upendo ndio msingi wa maisha yetu, je, itakuwa ni vigumu kuishika ile sheria ya Mungu katika viwango hivi viwili? 1 Yohana 4:20, 21; 5:2, 3.**

________________________________________

**10. Je, ni kwa sababu gani Paulo alirefusha huduma kule Troa, katika usiku wa siku ya kwanza ya juma? Alifanya nini katika siku iliyofuata ilipopambazuka? Matendo 20:7, 11.**

________________________________________

a) Katika Biblia, siku mpya huanza pale jua linapokuchwa, sio katika usiku wa manane, na ndivyo ilivyokuwa ya kwamba haya yalikuwa ni baada ya Sabato. Mistari mengi inaonesha ya kwamba Paulo aliabudu panapo Sabato; lakini katika tukio hili maalumu, maadamu alipasa kuondoka panapo mapambazuko, alirefusha hotuba yake hata usiku wa manane.
b) Kama Paulo angeiadhimisha Jumapili, asingefanya safari hiyo ndefu katika siku hiyo. Badiliko la siku ya pumziko haijatajwa hapa.
c) Waliumega mkate kila siku (Matendo 2:46).

**11. Katika kuwashauri kujiwekea kando sadaka kwa maskini kule Yerusalemu, je, Paulo aliwaeleza wale ndugu kukusanyika ama kujiwekea kando ile pesa? 1 Wakorintho 16:2.**

________________________________________

*Haisemi cho chote juu ya badiliko la siku ya pumziko.*

## *HAPANA HATA MSTARI MMOJA WA BIBLIA UNAOONESHA YA KWAMBA SIKU YA KWANZA YA JUMA INAPASA KUADHIMISHWA*

Hebu na tuangalie nukuu chache muhimu:

- Kadinali Gibbons aliandika: "Waweza kusoma Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, na HUTAPATA MSTARI HATA MMOJA UNAOIDHINISHA KUTAKASWA KWA JUMAPILI. Maandiko yanakazia maadhimisho ya kidini ya Jumamosi, siku ambayo sisi wala hatuitakasi."-The Faith of Our Fathers, toleo la 1917, uk. 72, 73.
- "Jumla ya wazo la kubadilisha siku ya kwanza ya juma mahali pa siku ya saba ya juma na kule kupisha, pengine katika namna ya kiroho, juu ya pumziko la Sabato lililosimama katika amri ya nne WALA HALIKUSIMAMA KATIKA MAANDIKO MATAKATIFU WALA KATIKA UKRISTO WA KALE." Smith and Cheatham, Dictrionary of Christian Antiquities, mada ya Sabato.
- Dr. Edward T. Hiscox, mwandishi wa Kanuni ya Wabaptist (Baptist Manual) alitoa tamko lifuatalo mbele ya kundi la wachungaji: "Kulikuwako na iko amri ambayo yapasa kuadhimishwa kama takatifu: hii Sabato, lakini siku ile ni Jumamosi na wala sio Jumapili. Kwa hiyo, yaweza kusemwa, ya kwamba Sabato ilihamishwa kutoka kwenye siku ya saba hadi kwenye siku ya kwanza. Ni wapi kule ambako usajili wa badiliko kama hili waweza kupatikana? Wala hakuna katika Agano Jipya, maadamu hakuna kabisa kinachohusiana na jambo hili." Kutoka kwenye kipengee kilichosomwa katika Mkutano huo wa Wachungaji kule New York, panapo Novemba 13, 1893.

## *MASWALI FULANI KUHUSU SABATO*

**12. Tunawezaje kufahamu kama Sabato hii ya leo ndio ile ambayo Mungu aliitakasa katika uumbaji? Je, hakujawa na badiliko katika kalenda?**

a) Tukiangalia katika kalenda ya Wakristo, Wa-orientali, Waislamu, Wakoptiki ama Wayahudi, tunaona kuwa miaka inabadilika, lakini Sabato inasalia kuwa ile ile. Katika kalenda ya Kiyahudi, mwaka 5778 ni sawa na mwaka wetu wa 2018.
b) Kalenda ya Juliani ilianza kunako mwaka 46 K.K. ikaja kusahihishwa mnamo 1582 na kubadilishwa jina kuwa ni kalenda ya Gregori; hii ndio tunaitumia hata leo.
Pale wataalamu wa elimu ya nyota walipogundua ya kwamba majira ya machipuo huanza katika nyakati tofauti; tarehe za kalenda zilisogezwa kwa siku 10 mbele, ilikuwa ni Alhamisi, Oktoba 4, watu walipokwenda kulala usiku na walipoamka siku ya Ijumaa ilikuwa ni Oktoba 15. Mzunguko wa juma haukubadilika.

c) Kuna vipande viwili vya ushahidi unaoonesha kwamba Sabato ni ile ile iliyotajwa katika uumbaji:
   1. Ule mujiza wa mana kule jangwani. Mungu anaijua ile siku aliyoitakasa. Mungu aliwapa kiasi mara dufu ya mana panapo Ijumaa na asiwape cho chote panapo Sabato (Kutoka 16:4-35). Mungu alifanya mujiza huu jangwani yapata mara 2000.
   2. Kristo pamoja na wanafunzi Wake walitunza Sabato (Luka 4:16; 23:54-56). Je, Mwana wa Mungu alitunza siku potofu kwa miaka 33?

**13. Paulo anaelezea juu ya Sabato gani anayoitaja katika Wakolosai 2:16, 17: siku za mapumziko zilizoamriwa, ambazo zilikuwa ni kivuli cha Kristo, ama ni ile siku ya saba?**

______________________________________________________________

*Katika ile sheria ya maadhimisho, iliyoandikwa na Musa katika kitabu (Kumbukumbu 31:24-26), kuna sikukuu saba za mwaka, ambazo zilitokea katika mwezi wa kwanza na wa saba. Sikukuu hizi (Pasaka, sikukuu ya Mkate Usiotiwa Chachu, Malimbuko, Pentekoste, Sikukuu ya kuzipiga Baragumu, Siku ya Upatanisho, na Sikukuu ya Vibanda) hizi zote ziliitwa pia ni Sabato ama siku za mapumziko. Hazikuwa na uhusiano na ile amri ya nne (Walawi 23:38, 39). Zilikuwa ni kivuli ama mfano wa Kristo.*

**14. Je, suala hili ni muhimu kiasi hicho? Je, haiwezi kuwa sawa ukiitunza siku nyingine yo yote? Je, tunaweza kuyatumainia maoni yetu? Mithali 16:25.**

______________________________________________________________

**15. Watu wengi huiadhimisha Jumapili; je, watu hao wengi waweza kukosea? Ni nani watakaopotea? Mathayo 7:13, 14.**

______________________________________________________________

a) Sio suala la kuungana na walio wengi ama wachache bali kuwa upande wa Yesu.
b) Watu wengi husema: "Wazazi wangu na mababu zangu siku zote wametunza Jumapili, nami sipendi kuwa tofauti." Je, ni nani ambaye Mungu atamlaumu na kumhukumu: ni wale waliotenda dhambi kwa kutojua ama waliotenda dhambi kwa kufahamu? Matendo 17:30; Yakobo 4:17.

## *HITIMISHO*

**16. Je, Biblia yawaitaje wale wanaorejeza Sabato kama siku ya pumziko? Isaya 58:12, 13.**

______________________________________________________________

**17. Je, Bwana anaiitaje Sabato na ni baraka gani ambazo tunazipokea katika siku hii? Isaya 58:13, 14.**

______________________________________________________________

***Uamuzi wangu:*** *Ninakubali kwamba Sabato ya Mungu imegeuzwa kwa hila na Jumapili, siku ya ibada za kipagani na iliyobuniwa.* ❏ *Ndio* ❏ *Hapana*

# 15 *VIWANGO VIWILI VYA UPENDO*



Hapana nguvu iliyo kubwa kuliko upendo. Ndilo jambo kuu lililopata kuimbwa na kuandikiwa zaidi na washairi. Ndio uwezo wa juu zaidi. 1 Wakorintho 13:13. Watoto wanahitaji upendo wa mama zao. Ndio unaowapatia maisha na kuwasaidia kukua kiafya. Upendo ndio unaomstawisha mtoto na tamanio la vijana. Watu wengi wamejiondolea maisha yao kutokana na mambo ya kukatisha tamaa! Hawakupenda na wala hawakujisikia kupenda. Upendo ndio mfumo mkongwe zaidi katika kumsaidia mwanadamu.

## *UPENDO UMEANDIKWA KATIKA DAMU*

**1. Je, Mungu aliwaachilia mbali viumbe Wake aliowaumba, licha ya kutokuwa na shukurani kwao? Luka 19:10.**

______________________________________________________________

**2. Mfano mkubwa zaidi wa upendo wa Mungu kwa mwanadamu ulikuwa ni upi? 1 Yohana 4:9-11.**

______________________________________________________________

**3. Je, twawezaje kuwa marafiki wa Yesu na kuonyesha upendo wetu Kwake? Yohana 15:14, 10; 14:15.** __________________________________________

*Hatuwezi kununua mbingu kwa njia ya matendo yetu. Wokovu ni karama ya Mungu (Wagalatia 2:16). Hata hivyo, wokovu ni ule utendaji wa Mungu "katika mwanadamu" kwa njia ya Roho Mtakatifu.*

**4. Iwapo tunataka kufuata mfano wa Kristo, tutendeje ili kuupata wokovu wa milele? Waebrania 5:8, 9.** ________________________________________

**5. Maana halisi ya amri hizi ni nini? Mathayo 22:37-40.**

*Kuna viwango viwili vya ____________________. Upendo ni ile nguvu inayokufanya umpende Mungu.*

*Je, ni kwa nini Mungu alimpatia Musa mbao mbili badala ya moja?*

- Katika ule ubao wa kwanza kuna zile amri nne za kwanza, ambazo zinatueleza juu ya namna ya kumpenda Mungu. Huu ndio upendo katika kiwango cha kwanza.
- Katika ubao wa pili, tunakuta amri sita za mwisho, ambazo zinahusu jirani zetu. Hiki ni kiwango cha pili cha upendo.

## *UPENDO KATIKA KIWANGO CHA KWANZA*

**6. Tunaonyeshaje upendo wetu kwa Mungu kwa kulingana na amri tatu za kwanza? Kutoka 20:3-7.**

a) Kumweka Mungu katika mahali pa kwanza; zaidi ya mambo yetu yote yanayotufaidia ya kidunia, majisifu yetu, heshima zetu binafsi, n.k.
b) Tusimwabudu kama vile tuonavyo sisi bali kama alivyoagiza Yeye, katika roho na kweli.
c) Tukilichukulia jina Lake kwa heshima na kicho.

**7. Tunaoneshaje upendo wetu kwa Mungu pale tunapoitunza Sabato? Kutoka 20:8-11.**

*Kwa kuziratibu kazi zetu za juma tangia siku ya kwanza ya juma ili kwamba tuweze kuiweka kando siku ya saba mahususi kwa Mungu. Tunakumbuka kwa shukurani juu ya kazi ya uumbaji wa Mungu kwa njia mbili (Zaburi 118:24):*

***Kimwili:*** *kufurahia amani katika siku ya pumziko kwa kuwako katika mazingira ya asili.*